# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report Of

# DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MAGHARINI CONSTITUENCY,

# HELD AT MAPIMO PRIMARY SCHOOL

ON

October 14, 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MAGARINI CONSTITUENCY, HELD AT MAPIMO PRIMARY SCHOOL**
**ON 14/10/02.**

**Present:**

Prof. Idha Salim - Commissioner
Asst. Programme Officer - William Opili
Verbatim Recorder - Gladys Osimbo

The meeting started at 10.10 a.m. with Com. Idha Salim in the chair.

**Com. Idha Salim:** Hamjambo nyote. Tungependa kuanza tumechelewa dakika kumi hivi na kwa kuwa kuna mengi ya kusema ningependa tuanze moja kwa moja na kama ilikuwa adha yetu ningependa kuanza kwa dua au maombi ambayo itatupa baraka ya kukamilisha kazi hii yetu kwa njia inayofaa. Yuko yeyote kati yetu anaweza kuja mbele hapa akutuombea. Tafadhalini, any volunteer.

**(Prayer)**

**Emmanuel Masha:** Tufunge macho kwa heshima ya Mwenyezi Mungu tuombe. Baba katika jina la mwanawe tunakushukuru, tunakuinua, tunakuabudu siku ya leo, Bwana hakika imekupendeza kutukusanya mahali hapa nikijua ni kwa mapenzi yako. Tazama bwana siku ya leo ni siku njema, siku nzuri ambayo kwamba umeichagua kwa ajili ya kurekebisha

Katiba ya nchi hii. Bwana wako uwe kielelezo siku ya leo, katumie fikra zetu na mawazo zetu ili bwana tukatende kitu ambacho kwamba kinaweza kutufaidisha katika maisha yetu. Bwana wangu uhusike Bwana, roho wako mtakatifu akaingia katika akili zetu ili Bwana tutakayotenda mfalme ikawa faida Bwana katika nchi ili Mungu wangu tukazidi kukuinua wewe na kukuabudu maana tunakutegemea wewe katika maisha yetu. Tunakuomba hayo machache Bwana nikijua kwamba umesikia na utajibu sawa na mapenzi yako katika jina ya Yesu Kristo Bwana tunakuomba na kushukuru. Amen.

**Com. Idha Salim:** Asante sana na sasa ningemuita District Coordinator wetu Bwana Kingi Jeffa, ajijulishe yeye na pia kwa kuwajulisha wananchi na wanakamati yake ambaye imekuwa ikifanya kazi ya kuhamashisha wananchi katika kazi hii ya Katiba.

**Kingi Jeffa (District Coordinator):** Hamjambo nyote. Nafikiri sisi si wageni hapa, tumekuja nafikiri hii ni mara yetu ya tatu. Kama mjuavyo katika sehemu hii ya uakilishi bungeni tuna committee ambayo inashughulikia mipango ya urekebishaji Katiba mashinani. Mimi naitwa Kingi Jefa ambaye ni District Coordinator wa Malindi. Kila sehemu ya uakilishi bungeni kuna Committee ya watu kumi, mmoja wapo ni mimi na Mbunge ambaye ni Noti Kombe, hajafika bado. Pia tuna mwanakamati ambaye katika ile committee tuna Chairman wetu ambaye ni bwana Jilo Oloto yuko hapa,. Katika sehemu ya Mambrui tuna wakilishwa na Fazia Hamed ambaye yuko pale, upande wa Magarini tuna Loise Kashuti, yuko hapa. Upande wa Fundisha tuna Mary Menza, yuko pale. Bwana Chilo upande wake ni Gongoni lakini anasaidiwa na councilor Akaku. Upande wa Adu tunaye James Kirimo nafikira bado hajafika. Upande wa marafa tuna Bwana Peter Thoya nafikiri yuko pale. Upande wa Garashi Gadambra tunaye Josphat Musanzu. Hao ndio wanakamati ambao wanashugulikia maswala ya Katiba katika sehemu hii ya uakilishi bungeni.

**Com. Idha Salim:** Asante sana Kingi kwa kutujulisha na wanakamati na mimi ningependa kuwajulisha na wale ambao wametoka Nairobi na mimi. Jina langu mimi mwenyewe ni Ahmed Idha Salim, mwanatume na pia ni naibu wa mwenyekiti wa Tume. Kwa upande wangu wa kulia pale yuko William ambaye kazi yake ni muhimu sana kusajili na kuandika yeyote ambaye itazungumzwa hapa kadri iwezavyo kwa karatasi na kalamu. Lakini kwa upande wangu wa kushoto pale yuko Gladys, yeye kazi yake ni kuandika na pia muhimu zaidi ni kunasa kila neno litakalosemwa kwenye tape ili kuhakikisha kwamba yote ambayo tutawaeleza na yale maoni yenu juu ambayo tutawaeleza yatanaswa. Itafanyiwa rekodi na tukirudi Nairobi yatachapishwa kwenye karatasi na kuwa ni sehemu ya rekodi ya kazi hii nzima ya Tume ili kwamba vizazi vijavyo baadaye baada ya miaka ishirini, mia moja, mia moja na hamsini tuombe waweza kusoma iliyozungumzwa hapa Magarini tarehe hii ya leo neno kwa neno. Kwa hivyo tusipoteze tena wakati.

Mimi nimekuja hapa na wenzangu kutoka Nairobi kwa kazi muhimu sana. Mmetupa sisi wanatume kazi ya kuandika hii Katiba na mkatuambie tuandike kufuatia maoni yenu wala la, tulipokuja hapa awali. Sasa kazi hii tumekamilisha kadri tulivyoweza. Tumeandika mswada wa Katiba, nafikiri neno hili mswada lafahamika, mswada ni draft. Hii maanake ni kwamba ni draft, haijawa Katiba lakini mswada ni draft iliyoandikwa na baadaye ikipitishwa kwa Katiba ndio itakuwa sheria yetu kubwa hapa

nchini na Katiba yetu mpya. Sasa kutokana na kazi hiyo ya kuiandika Katiba, kabla sijaendelea ningependa kumkaribisha Bwana DO wetu, Henry Wafula, ambaye na shughuli zake zote amewahi kuja hapa kutukaribisha na tumejikaribisha Bwana Wafula na hivi sasa unaweza kutukaribisha kirasmi kabla haujaendelea na kazi zako zingine. Bwana Wafula karibu.

**Henry Wafula (DO):** Asante Prof. Idha Salim, sijazoea kuongea kama nimeketi. Basi Prof. Idha Salim, Bwana Oloto, Bwana Kingi na wananchi wa Magarini constituency hamjambo? Hamjambo tena?

**Audience:** Hatujambo.

**Henry Wafula (DO):** Nafikiri ningependa--- hivi leo sio siku yetu, ni siku ya mwalimu wangu wa zamani. Huyu Professor alifundisha University ya Nairobi, kwa hivyo nilimwambia alivyokuja ofisini karibu kwa sababu mimi ni product yake. Kwa hivyo yeye ananijua na nimesema amekaribishwa Magarini. Professor wananchi wa hapa ni wazuri hawana mambo mengi,watakueleza maneno ya Katiba yote, yangu ni kusema tu muendelee niko na kazi nyingi, Oloto ameleta kazi nyingi kweli kweli. Kwa hivyo leo ni siku ya Constitution, mimi nitawaambia muendelee hata kama ni saa kumi na mbili Prof. mimi ni kijana wako unajua, ujusikie uko nyumbani. Kwa hayo machache, asanteni.

Asante sana Bwana DO Wafula kwa kutukaribisha kwa njia yako hiyo ya moyo kabisa na tumefurahi sisi kufika hapa. Nilikuwa nishaanza kueleza wananchi madhumuni ya sisi kuweko hapa. Madhumuni yake kama nilivyosema ni kuhakikisha kwamba maoni yenu yale haikupotea na kuja kuwaeleza tumeandika jambo gani katika mswada huu wa Katiba. Wenzangu wanakamati na pia District Coordinator wameshwapa nakala or copies ya hiyo Constitution, imetoka kwa lugha ya Kiswahili hivi sasa kwa kuwa hapo awali ilikuwa na lugha ya Kiingereza. Na kuna vitu viwili kwa hakika hapo mbele yenu; kuna kwanza hiyo mswada wa Katiba, pili kuna taarifa yetu au report ya kazi tuliyoifanya. Tumepewa kazi gani tumeeleza hapo, ni kile kitabu rangi kijani nafikiri kila mmoja wenu anacho copy yake. Basi hapo kuna maelezo ya juu ya jinsi tulivyofanya hii kazi. Tumeeleza tumeambiwa tufanye kitu gani tutoke, tuzunguke kila Constituency tueleze wananchi maoni yao juu ya mambo tofauti tofauti yanayohusu Katiba. Pia tuliwapa mtakumbuka vijitabu vidogo maswala na maswali, sawa? Na kufuatia kitabu hicho na yaliyomo mliweze kutupa maoni yenu juu ya sehemu mbali mbali ya Katiba.

Sasa kama nilivyosema tumeshaandika mswada wa Katiba, mtaisoma kwa makini wale ambao hawajapata nafasi. Nafikiri wengine wameshaelezwa yaliyomo kwa njia ya radio na kadhalika na mmesikia mengi juu yake. Sasa leo ni kazi yangu mimi kirasmi kama ilivyo kazi ya wenzangu walioko hivi sasa kila sehemu ya nchi yetu wakiwa na vikao kama hivi, kuwaeleza wananchi juu yaliyomo katika hii Katiba. Baada ya kumaliza kuwaeleza kadri niwezavyo yaliyomo kwa maana ni Katiba ndefu. Yaliyomo ni mengi, lakini tutashikilia yale ambayo nafikiri ni muhumu zaidi ambayo mngependa kupata maelezo yake kwa urefu. Baadaye mtatuuliza maswali juu yake kutaka kujua kuelezwa zaidi au kusema jambo hili sisi hatuipendelei tungependelea jambo lile au lile na kadhalika. Hii ni Katiba yenu, kwa hivyo mwishowe itakuwa ni Katiba ambayo itapitishwa kwa njia yenu nyinyi na maoni yake juu yake na pia kwa njia ya wakilishi wenu.

Tukishamaliza kazi hii ya kuwaeleza yaliyomo mimi na wenzangu kule Nairobi na Commission tutatayarisha mkutano mkubwa unaoitwa National Constitutional Conference au mkutano mkubwa unaohusu Katiba wa taifa nzima. Na katika conference mkutano huo watakuweko na wawakilishi zaidi ya mia siti, kati ya mia sita na mia saba. Wote hao watakaa watajadiliana juu ya mswada wa Katiba na huenda wakabidilisha mengi au kidogo hatujui, inategemea jinsi ambavyo mkutano utaendelea. Kila fungu katika Katiba litajadiliwa ama itabakishwa ilivyo watapitisha ibakie vile vile au watabadilisha hapa na pale. Kwa hivyo mwishowe mswada wa Katiba utabadilika kwa njia fulani. Mkutano ukishamaliza kazi yake, itarudi kwetu na tutaiandika sasa kufuatia mapendekezo ya mkutano huo mkubwa wa wakilishi mia sita na hamsini hivi na kisha ikiwa tayari tutampa Attorney General ataipeleka bungeni na bunge tena itajadiliana juu yake na kwa kuwa wabunge watakuwemo katika huo mkutano mkubwa wa mia sita na hamsini hatutaraji kuwa watapinga jambo lolote. Ikifika kule itakuwa ni kuipitisha moja kwa moja na hapo ndio itakapokuwa ndio Katiba yetu mpya.

Labda mgependa kujua ni nani hao wakilishi. Wakilishi watakuwa ni wabunge wote, juu yao watakuweko pia wanatume wote kina sisi ishirini na tisa. Pia watakuwemo wawakilishi watatu kutoka kila district, Malindi district wakilishi watatu, Mombasa district watu watatu na kadhalika. Kwa hivyo kutakuwa na wawakilishi tatu katika hesabu ya mia mbili na kumi, wawakilishi kutoka kila district. Kisha kutakuwa na uakilishi katika kila dini ilioko hapa nchini, Kiislamu, Kikristo, Kihindu na kadhalika. Kisha kutakuwemo pia wakilishi wa akina mama, wakilishi wa walemavu, wakilishi wa wale ambao tunawaita marginalized, waliowekwa kando mpaka sasa hawajapewa nafasi ya kushiriki kikamilifu katika maisha yetu ya kiuchumi au maisha yetu ya kijamii sawa sawa au maisha yetu ya kisiasa. Kwa hivyo wote hawa watakuweko kwa huo mkutano mkubwa na kama nilivyosema wakishapitisha kujadiliana na kupitisha mswada wa Katiba itakwenda mbele Parliament ipitishwe iwe ndio Katiba yetu kubwa. Kwa hivyo hizo ndizo stages zilizobakia kabla ya mswada huu wa Katiba kuwa ni Katiba yetu mpya.

Sasa hebu tuitizame hii Katiba au mswada wa Katiba, nitapitia sura zake kadha wa kadha na kueleza kwa ukamilifu kadri uwezavyo maana wakati ni mfupi sana kueleza kila neno lililoko hapa. Lakini baadaye bila shaka mtaisoma nyinyi wenyewe na mkiwa na maoni yeyote mnaweza kutupa maoni yenu hata kuandikwa kwa njia ya district coordinator wetu au wanachama wa kamiti yetu na hao watatupelekea Nairobi, tutabaki nazo na saa zile mkutano mkubwa wa National Constitutional Conference ukishamaliza tutatizama maoni yenu, juu ya mapendekezo yao na maoni yao na kuimaliza hii Katiba kwa njia ya kimwisho kabisa, in a final way.

Sasa hebu tutizame yaliyomo. Ukitizama mswada huu wa Katiba utaona kwamba tuna sura au juzu au chapters ishirini. Chapter zingine ni fupi sana na nyingine ni ndefu. Kabla ya sura ya kwanza tunaanza na kitangulizi – preamble. Katiba yetu ya sasa haina preamble, lakini tungependa kwamba tuwe na preamble katika Katiba yetu mpya. Preamble au kitangulizi ni muhimu sana, inasema kwa ufupi kabisa; kwamba sisi wananchi ndio wafalme wa nchi. Sisi ni wenyeji, sisi ni wenye kumiliki nchi yetu na yote na kila kanuni lazima itoke kwa wananchi, yaani nguvu za mwananchi au wananchi ndizo zinazosisititzwa katika preamble na juu ya hayo tunasema kwenye preamble. Pia ni vipi tungependelea serikali iendeshwe na vipi awana gani ya

serikali tungependelea kuwa nayo. Kwa hivyo kwa ufupi ukitizama ni fupi sana, inasema kwa Kiingereza; "We the people of Kenya". Unaona tunaanza na watu, hii ni sisitiza umuhimu wa raia katika nchi. "We the people of Kenya, aware of our ethnic, cultural and religious diversity and determine to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation, committed to nurturing and protecting the well-being of an individual, the family and the community within our nation, recognizing their aspirations or our women and men for a government to base on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law. Exercising our sovereign and inable rights to determine the formal governance of our country and having fully participated in the Constitution making process, do adopt, enact and give to ourselves and to our future generation this Constitution. God bless Kenya".

Kwa wale ambao kwa jumla hivi tumesema nini kwenye preamble tunasema; "sisi raia wa Kenya tukiwa tunajeriki tofauti zetu za kikabila, kiutamaduni na za kidini na tukiwa na nia ya kuishi pamoja kwa amani na umoja kama taifa moja isioweza kugawanyika, tukiwa pia na azma kubwa ya kushtawisha na kulinda hali nzuri ya kila mmoja wetu, kila familia na kila jamii, tukiwa pia tukitambua matakwa ya akina mama na wanaume ya kupata serikali ambayo msingi wake ni maadili ya kidharura ya uhuru, demokrasia, uadhilifu ya kijamii na utawala wa sheria. Tukitumia haki yetu ya ufalme wetu sovereignty na haki yetu isoweza kuchukuliwa na yeyote kuchagua aina ya serikali tunayopendelea kuipa nchi yetu, na kwa kuwa tumeshiriki katika kazi ya kurekebisha Katiba (nyinyi mlishiriki kutoa maoni yenu au sio), sisi tumekata shauri kuipokea hii Katiba, kuifanya ndio sheria yetu na kujipa nafasi yetu sisi wenyewe kwa hivi sasa na pia kuipa vizazi vizazi vijavyo. Mungu aibariki Kenya". nafikiri tumefahamu yaliyomo hapo. Ni fupi lakini ni muhimu sana, kama ambavyo sura ya kwanza pia ni muhimu.

Sura ya kwanza ni fupi sana mkitizama, chapter one; "Sovereignty of the people and supremacy of the Constitution". Ni fupi lakini ni muhimu sana kama ambavyo sura ya kwanza pia ni muhimu. Sura ya kwanza ni fupi sana mkitizama chapter one, sovereignty of the people and supremacy of the Constitution.

Sovereignty of the people: Neno hili sovereignty, sijui kama kuna neno bora zaidi kwa lugha ya Kiswahili, ni ufalme wa watu. Watu kuwa ni wafalme, yaani ndio watawala. Pili, Supremacy of the Constitution. Katiba iwe ni juu ya kila kitu ndio ikaitwa kanuni kubwa ya nchi yeyote. Kwa hivyo tunasema kwamba watu ndio sovereign na tukisema kuwa watu ni sovereign maanake wao ndio watakao kata shauri juu ya jambo lolote muhimu ambalo linaohusu maisha ya kijamii, maisha yao ya kiuchumi, maisha yao ya kisias. Wao ndio watakaochagua watumishi wa serikali, sio kwa njia ya moja kwa moja lakini kwa njia nyingine. Ndio wao ambao watakaowachagua wajumbe katika Bunge, "huyu tunamchagua akuwe Mbuge wetu aende akatufanyie kazi na kadhalika". Hii ndio kazi kubwa ya kusema kwamba sovereignty is the people.

Pia supremacy of the Constitution; Katiba umuhimu yake ni kwamba ndio kanuni au sheria kubwa katika nchi yeyote. Kanuni yeyote nyingine au sheria yeyote nyingine huwa ni chini ya Katiba na ikiwa mkishaifahamu hii Katiba kutatokea jambo lolote au kanuni yeyote ambayo mnasema kwamba kanuni hii inagongana na sheria. Mtu anaweza kwenda kortini akashtaki kanuni hiyo kwamba hii sio kanuni ya sawa, hii si halali maanake inagongana na sheria. Na ni muhimu kwa mwananchi kuifahamu hii Katiba

na kufahamu yaliyomo ili kuweza kujua jambo lolote litakalofanywa ambayo inagongana na hii sheria kwamba hii si sawa na anaweza mtu kuchukua hatua ya kwenda kortini au mahakama akajadiliana kwamba jambo hili liondolewe au kanuni hii si ya sawa maana inagongana na Katiba. Katiba is the last resort (reference), unaregelea Katiba katika kila kanuni yeyote nyingine. Sasa hiyo ndio sura ya kwanza, sovereignty of the people, umuhimu wa watu katika nchi na kwamba watu ndio wana hakika kutawala nchi na supremacy of the Constitution na ukubwa wa Katiba iwe ni juu ya sheria yeyote nyingine.

Sura ya pili inaitwa 'The Republic' au Jamhuri, pia ni fupi lakini ni muhimu. Katika Katiba yetu ilioko hivi sasa tunaisifu Kenya kwamba ni republic au ni jamhuri, lakini hatuelezi kwa nini inaitwa jamhuri haitui kitu chochote nyingine. Jamhuri ni neno la kiarabu asli yake, ambayo imeingia katika lugha ya Kiswahili, maana yake ni watu kwa au raia jamla. Kwa hivyo tukisifu Kenya kwamba it is a republic Kenya ni jamhuri, maana yake ni hayo ambao walioeleza wale, maana yake ni watu ambao ndio kitu muhimu katika nchi ile na matakwa ya watu ndio muhimu, mapendeleo ya watu ndio muhimu. Kwa hivyo tunasema kwamba Kenya ni republic na kwa nini inatiwa republic na watu ndio muhimu? Zama za zamani na Bwana DO wetu ambao amesoma historia na mimi huko University of Nairobi, atajua kwamba zamani Wagiriki walikuwa wakijihukumu kwa njia ya wajumbe wa watu, wanasemea watu na wote wale wajumbe walikuwa ni sawa, hakuna mmoja ndiye bora kuliko mwenzake. Kwa hivyo watu katika nchi ya ugiriki zamani ndio walikuwa muhimu na kutumikiwa na wajumbe wao. Kwa hivyo pia tangu siku zile mpaka leo, utaona kwamba nchi yote ambayo imejisifu au kujieleza kuwa ni republic inaendesha serikali yake kufuatia maadili fulani, certain principles.

Ikiwa haitafuatia maadili hiyo, basi huwa si republic, basi huwa ni ufalme, monarchy au kitu kingine dictatorship kama siku za Urusi zamani au China zamani. Na maadili hiyo ya republic nini maana nchi yeyote ambayo inajisifu kuwa ni republic utaona maadili yake ni ipi. Ikiwa inafuata maadili hiyo basi hiyo ni republic. Maadili yenyewe ni vipi? Kwanza huwa utawala wake utawala mzuri kufuatia siasa ya vyama vingi. Haya ni maadili moja. Ikiwa nchi hiyo ina vyama vya kisiasa vingi basi hiyo ni ishara kwamba hiyo ni republic, lakini haya yatoshi. Pia iwe ni utawala ambao unashirikisha wananchi, wananchi wanashiriki katika kujitawala. Wanaweka watu kuwafanyia kazi kama wabunge, lakini watu wanashiriki kwa njia tofauti tofauti. Ukimchagua mjumbe au mbunge huwa ameshiriki katika utawala huo, usipompata kesho ukamuondoa ni kuonyesha una nguvu, una mamlaka. Kwa hivyo wewe unashiriki katika ile kazi ya nchi yako kuendeshwa.

Kwa hivyo maadilii mengine au ishara ile ya pili ni kwamba nchi hii ni jamhuri ni kwamba watu wanashiriki katika serikali yao. Popular of public participation in governance or participatory governance, utawala ambapo watu wanashiriki katika utawala huo. Pia jamhuri lazima iwe na transparency, iwe ni wazi, transparency ni tuseme kitambara ambacho unaweza kuona ndani yake. Kwa hivyo hii ni serikali ambayo unaweza kuona inavyoendeshwa; inaendeshwa vizuri, haindeshwi vizuri, imekwenda kombo hapa lazima istahishwe hapa na kadhalika. Na unaweza kusema na kueleza mambo haya hayaendeshwi vizuri, unaendeza mambo vibaya. Kwa hivyo jamhuri lazima iwe ni transparent, serikali ambayo unaweza kuiona sawa sawa. Pia accountability ni ishara muhimu ya jamhuri yeyote, yaani wale ambao wanafanya kazi katika serikali hiyo, unaweza kuona wanakupa hesabu mwisho wa mwaka, tumefanya hivi tumefanya vile katika eneo lile tumejenga barabara mbili tatu, tukajenga

na shule. Wanani wanarudi kwa raia na kusema waliofanya, 'Matumizi yetu ya pesa tulikuwa na pesa kiasi fulani tukatumia kiasi hivi hapa, kiasi vile pale, imebaka pesa tulizo nazo sasa ni kadha'. Hiyo ni hesabu sio? Wale ambao pia wanaamini wanaumanifu wa dini yeyote, Kristo, Kiislamu pia wanajua kwamba hesabu Mwenyezi Mungu atakufanyia hesabu siku moja. So serikali ya nchi yeyote ambayo inatoa hesabu yake mbele ya wananchi, hiyo ndio serikali ya kijamhuri maana wananchi wanajua jinsi ambavyo pesa yao au mali yao inatumiwa na wanaweza kukata shauri mwishowe matumizi ni mazuri. Hiyo ni maadili ya serikali ya kijamhuri.

Pia serikali ya kijamhuri inaheshimu haki za binadamu, jambo muhimu hiyo na akatoa uhuru wa kimsingi kwa kila mwananchi na pia una utawala wa kufuata sheria. Maana saa ingine unaweza kupata utawala katika nchi lakini haifuati sheria, mtu haki zake za kisheria zinavunjwa, lakini serikali ya kijamhuri lazima iwe ni serikali ambapo haki za kibinadamu zinaheshimiwa na pia utawala wake ni kufuata sheria. Askari polisi havunji sheria, Bwana DO pia anafuata sheria, Bwana DC anafuata sheria, Rais mwenyewe anafuata sheria hafanyi jambo vidi ya sheria. Ndio haya ambayo tunazungumza katika sura ya pili, the republic au jamhuri. Mtasoma wenyewe baadaye maelezo zaidi juu ya jambo hilo.

Sura ya tatu au juzu ya tatu or chapter three, pia inazungumizia mambo muhimu sana; 'National goals, values and principles', shabaha za kitaifa, malengo ya kitaifa, maadili ya kitaifa. Wajua serikali yeyote au utwala wowote lazima uone maadili, maadili ni values, mtu anataka hali ya ustawi wa juu katika maisha yake yote, sio? Kwa hivyo anafuata njia fulani au desturi fulani kumuongoza. Kwa hivyo kila nchi lazima iwe na values, tutaongozwa na maadili gani katika nchi yetu. Kwa hivyo mkisoma hapo mtaelezwa ni shabaha gani tunazo sisi tukiwa jamhuri ya Kenya na tunafuata maadili gani katika kuendesha maisha yetu ya kiuchumi, maisha yetu ya kijamii, maisha yetu ya kisiasa na kadhalika.

Tumeeleza kwa wingi tuna maadili labda kumi na tano hivi, mkisoma mtafahamu. Nitataja machache ambayo ni muhimu. Tunasema serikali itaendeshwa kwa njia iliowazi kama tulivyoelezwa, hapa pia tunasisitiza uwazi wa serikali wafanyi kazi wa serikali wawe accountable, wanatoa hesabu ya kazi yao tupate kupima ikiwa kazi yao wanaendesha uzuri au la. Serikali ya jamhuri itaheshimu, sikuheshimu pekee yake, itaheshimu na italinda na pia itastawisha haki za kibinadamu na uhuru wa kila aina ambayo mwananchi atakuwa nazo kama haki zake za kuzaliwa nazo. Hayo ni maadili pia, tunataka serikali ambayo inaheshimu na inalinda, mtu akiingilia haki zako serikali inalinda. Na kustawisha, kuendelesha mbele zaidi, haki zaweza kubakia pale pale lakini pia zinaweza kushtawishwa zaidi, ni kama mtoto. Utamlelea lakini utampa nguo lakini pia utaweza kumpa na vitamins kidogo apate kukuwa kwa na nguvu zaidi. Kwa hivyo haki zaweza kulindwa na kustawishwa katika nchi yetu.

Maadili mengine; serikali itaendeleza umoja wa taifa na kustawisha adhimio la wananchi kuwa na roho wa uraia mkubwa zaidi. Kama tasemavyo nchi yetu ni moja, ingawa tuna makabila tofauti tofauti, dini tofauti na kadhalika, lakini lazima tubakie na ile roho ya kutaka kuwa taifa moja. Kwa hivyo ni kazi ya serikali na ni shabaha yetu, tunasema katika huu mswada ni shabaha ya serikali kushtawisha ile roho ya wananchi kuhisi ule uraia kwa nguvu zaidi – wawe patriotic, wawe wanapendelea nchi yao, wanashikamana pamoja kuendelesha nchi yao kama raia wa nchi moja. Hiyo pia ni goal au shabaha kubwa ya hii Constitution.

Pia shabaha na maadili mengine; serikali itajilazimu na ni kama kutoa ahadi, utaahidi wananchi kwamba utaleta uadilifu wa kijamii na pia kuwapa wananchi haki zao za kimsingi. Nafikiri tunafahamu hapo. Pia inasema maendeleo na ustawi kwa kila sehemu ya nchi bila ya ubaguzi na kutumia mali ya umma au taifa kwa uzuri na kwa uadilifu ni wazi. Siku zile tukizunguka kupokea maoni yenu na kila kitu tulipata mashtaka mengi, "eneo letu halina shule za kutosha, eneo letu halina clinic za kutosha au maji tulionayo ni machafu, watoto wanapata ugonjwa baada ya kunywa maji hayo na kadhalika. Kwa hivyo tungependelea kwamba zile pesa zetu, mali yetu ya kiasili, aina mbili ya mali ya kiasili. Mali ambayo inaingia kwa njia ya kodi na kadhalika na kuenda treasury, to tax department na kila kitu. Kisha kuna mali ya asili; pori zetu, wananyama wetu wa porini, mali yetu ya baharini na kadhalika, kunapato hapa pia. So tunasema kwamba mali yetu ya kiasili lazima itumiwe kwa njia ya uadilifu wa kijamii. Kila eneo letu la Kenya lazima ipate sehemu yake ya mali hiyo ipate kuendelea kijamii na kiuchumi na kwa kila njia na pia kila mwananchi apate haki zake za kimsingi. Tutataja baadaye haki hizo za kimsingi. Hayo ndio yaliyomo katika sura ya tatu, shabaha au malengo na maadili yetu.

Sura ya nne; Citizenship, uraia, ni nani ambaye ana haki ya uraia, ni nani ambaye anaweza kuzingatiwa huyu ana haki ya kiuraia. Na pia tunasema kwamba, tukisema kwamba hawa ni raia basi raia wote ni lazima wapate kuzingatiwa kuwa ni sawa kabisa, akiwa ni mwanamume akiwa ni mwanamke akiwa ni kabila hii au kabila ile na kadhalika. Sote ni sawa. Equally all citizens of Kenya are equally entitled to the rights, privileges and benefits of citizenship. Kila raia wa Kenya ana haki sawa sawa na mwenzake, ana faida sawa sawa na mwenzake raia na pia ana wajibu ule ule wa raia. Tuna haki na tuna wajibu pia sio? Haki saa zingine huenda na uajibu wake mtu, lazima utimize hili na lile ikiwa wewe ni raia, si kuwapata tu lakini pia unatoa pia kwa wenzako haki fulani au una wajibu wako pia. All citizens of Kenya are equally entitled to a Kenyan passport and to any document of identification issued by the state to citizens. Kila raia ana haki automatic, wewe ukiwa raia basi huna haja ya kuomba au kueleza kwa nini unataka passport, ni haki yako, It is no longer a privilege.

ID: Ikiwa ile ID inatakikana katika nchi basi kila raia ana haki ya ID. Hana haja ya kueleza, hana haja kumbembeleza, hana haja ya kutoa kitu chochote chai kupata hiyo ID ni haki yake na asipopewa haki yake anaweza kuenda akashtaki. Tutaeleza baadaye atashtaki wapi, tumeweka baraza fulani, tumeweka watu fulani ambao kazi yao ni kuhakikisha kwamba haki ya kila raia, haki ya mwananchi zafuatwa. Kwa hivyo kuna njia tofauti tofauti sio moja tu ambayo mtu ataifuata ili kushikilia haki yake.

Pia tunasema kwamba uraia mtu anaweza kupata kwa njia fulani; kwa njia ya kuzaliwa. Kwa hivyo yeyote ambaye atazaliwa nchini maadam mzazi wake mmoja ni Mkenya basi huyo amepata uraia. Sio lazima wawe ni wazazi wawili, hata mmoja ikiwa ni mama au baba, Ikiwa ni mama na baba sawa. Ikiwa ni baba tu Mkenya, mama si Mkenya ni Mtanzania tuseme au Mganda, anapaswa haki ya uraia. Pia anapata uraia kwa njia ya kuishi nchini, registration, amekaa muda fulani nchini hapa Kenya, alikuwa ni mtu wa nje lakini amekaa Kenya kwa muda usiopungua miaka saba. Baada ya miaka saba huyo akipendelea kuwa

raia wa Kenya na ikiwa alikuwa na tabia nzuri na kadhalika hakuwa mtu ambaye alikuwa analeta madhara nchini anaweza kujiandikisha akaomba akapewa uraia na kadhalika. Tumeeleza hapo. Pia tumeeleza kwamba Mkenya akimuoa mtu wa nje, yule mumewe au mkewe wa nje pia anapata uraia. Hivi sasa Mkenya mwanamume akimuoa mke kutoka nje, yule mkewe anapewa uraia hivi sasa, lakini kina mama wakapiga kelele kuna ubaguzi. Ikiwa Mkenya mwanamke amemuoa mwanamume wa nje kwa hivi sasa yule mumewe hapati uraia. Tumesema ubaguzi huu uondolewe. Mkenya yeyote atakayemuoa mtu wa nje, huyu mumewe au mkewe anaweza kupata uraia. Si mke tu lakini pia mume wa Mkenya ana haki ya kupata uraia. Mtaelezwa zaidi mkisoma mtapata maelezo zaidi juu ya mambo haya ya uraia ili tuendelee mbele ni mengi ya kusemwa na samahani naenda mbio mbio lazima baadaye tutaweza kuelezana zaidi ikiwa kuna swala yeyote.

Sura ya tano pia ni muhimu, inaitwa 'The Bill or Rights' (kanuni ya haki). Haki ni kitu muhimu sana au sio. Saa zote tukilalamika tunaona kwamba tunaonewa hivi au vile, tunafikiri au tunaamini kwamba tuna haki fulani lazima tupewe. Sasa sura hii ya tano mtaona ni ndefu na ninaambiwa na wenzangu ambao wanahusika na mambo haya, wamesoma zaidi, yangu ni kwamba yaliyomo katika sura hii ni mengi kuliko yaliyomo katika sura kama hii katika Katiba ya nchi nyingi sana ulimwenguni. In other words they have given or concentrated on the rights of the Kenyan more than many other countries, tumetoa kila aina ya haki katika hii kanuni ya haki ya mwananchi. Ni ndefu nilivyosema lakini mtaisoma kwa makini baadaye maana mmeanza kupata. Lakini hebu nieleze machache. Tunasema hapa kwa mfano kuna haki moja, tunasema serikali itachukuwa hatua za kuweka sheria zinazohitajika ili kuwapatia wananchi haki za kimsingi. Haki za kimsingi ni zipi? Haki ya chakula, hii ni haki ya kimsingi sio? Bila chakula binadamu hawezi kuishi. Chakula, matibabu pia kupata ugonjwa hawezi kupata matibabu ya kimsingi, elimu ya msingi hiyo ni haki. Maji masafi, mashtaka haya ya maji mabaya tumeisikia mahala pengi sana. Makao, mtu asilale barabarani, anaweza kupata makao na amani yake ya binafsi na ya mali yake, amani ni kitu muhimu. Kwa hivyo mtu atataka kwamba hii si kwamba anaishi anapata basic needs, haja zake zile za kimsingi na pia analala kwa amani katika nyumba yake au shamba lake bila kuwa na hofu maana ni wajibu wa serikali kwamba ulinzi wa raia uwe unashtawishwa.

Baada ya kupendekeza kwamba haki za kimsingi zipewe mwananchi tunaeleza kwengine kule mwisho kwamba kuna kanuni Fulani, tumesema hapo awali kwamba serikali itachukua hatua za kuweka sheria sio? Hii maanake kwamba kuna sheria fulani ambazo hazijawekwa, kuna haja za kuziweka sheria hizo. Na mkitizama kule nyuma kabisa katika mswada wenu wa Katiba mtaona kwamba tumepewa time frame, viwango vya wakati. Kwa hivyo tumesema kwamba hizi basic needs zisiwe na kiwanago, hatusemi kwamba kila mwananchi baada ya miaka miwili aweshapata yote hayo. Tunasema kwamba serikali ianzishe hatua ili mwananchi apate haki hizi, lakini hatusemi kwamba baada ya mwaka moja ati kila mmoja wetu awe na nyumba, kila mmoja wetu awe na matibabu ya kutosha, kila mmoja wetu mtoto wake anapata elimu ya bure ya kimsingi na kadhalika. Maana tunajua kwamba serikali inapato lake inatoka hapa hapa nchini kwa njia ya kodi na mali ya asili na kadhalika. Kwa hivyo tunaipa serikali muda kwanza, hii safari ya kutupa sote haki zetu za kimsingi lakini ianze hiyo safari. Safari lazima ianze na tunasema kwingine kwamba rais wa nchi atakuwa akitoa report kila mwaka katika bunge kutupa repoti jinsi ambavyo mambo inaendelea, progress report. Apate kuwaeleza kwa mfano haki ya kila mwananchi ya kimsingi vipi imetimizwa, tumefika wapi, tumebakia na nini na ni kwa nini tumechelewa kutoa haki hii au ile. Kwa hivyo tumeona kwamba

lazima to be realistic, hatutaraji kwamba tuna pesa za kutosha yote haya tunafanya kesho au kesho kutwa tutakuwa na progress na kutakuwa na reporting juu ya mambo hayo.

Pia tunasema katika Bill of Rights kusiwe na ubaguzi katika nchi yetu wa kikabila, wa kijinsia. Ubaguzi kati ya mwanamume na mwanamume wakiasili, huyu asili yake ni fulani kwa hivyo huyu sio sawa na mimi au kwa rangi huyu ni rangi fulani na mimi ni rangi Fulani. Au wa umri, kusiwe na ubaguzi wa umri kwamba hawana haki kama mimi kijana na kadhalika. Au uzima, mimi ni mzima yule ni mlemavu kwa hivyo haki zangu mimi ni zaidi. Hakuna ubaguzi kati ya mwananchi kufuatia yote hayo au dini, hakuna aliyo bora, dini zote zitakuwa ni sawa mbele ya Katiba. Pia tunasisitiza haki za wa wazee kwa hivi sasa katika kuzunguka tumepata malalamiko mengi wazee wanasema kwamba--------(end of tape) na tunaju jinsi ambavyo thamani ya pesa imepungua sana au la? Kwa hivyo wazee wanapata taabu na wale ambao hawana kazi kabisa watoto wao wamefariki hawana mtu wa kuwatunza tunahaja ya kufikiria hali zao na kwamba wataendelea na kumaliza maisha yao kwa njia ambayo ni ya heshima si ya udhalilifu. Mzee kufa mtu hajui amekufa na nini na hakuna watu wake watakayemzika na kadhalika. Kwa hivyo kuna haja ya serikali na jamii pia kufikiria hali ya wazee kuishtawisha zaidi.

Haki za watoto: Tumesisitiza haki za watoto kwa njia ya kirefu kuliko hapo awali. Mtoto kulelewa vizuri na wazazi wake, kuvishwa, kuelemishwa, kutolazimishwa kufanya kazi. Tunajua wazee wengine wanalazimisha watoto kuzurura hapa na pale kuuza njungu, kuuza hili au lile ili jamii yake ipate mapato ya kutosha kwenda kununua mkate na maziwa, ni ukweli. Taabu hiyo saa nyingine inamlazimisha mzee kufanya hivyo, lakini tufanye kwa njia ambayo haitamdhuru yule mtoto, haitamnyima elimu, haitamnyima kupumzika kwa kutosha. Mchana mzima mpaka jioni yuko nje anafanya kazi na tunajua kwamba kuna wengine tunajua kwamba wengine pia wanapigwa vibaya na wazazi wao. Kwa hivyo kuna haja ya kulinda hali ya mtoto aishi kwa njia inayofaa.

Walemavu: Tumezungumzia walemavu na haki zao mtaona hapo. Haki ya privacy, privacy ni kitu muhimu sana, mwananchi akiingia nyumbani kwake anajua hapa mimi sitaingiliwa na mtu yeyote wakati wowote kwa ati tumesikia nyumba yako ina hivi na vile. Askari anaingia tu bila ya warrant, bila ya amri au haki ya kuingia nyumbani kwake. Nyumba yake mtu Waingereza wanasema, "an English man's home is his castle" na nyumba ya Muingereza ni ngome yake kama tuseme Fort Jesus, maanake awe amelindika, amejilinda huko hakuna atakayemuingilia kwa urahisi. Kwa hivyo haki ya mtu kutoingiliwa, tumetilia mkazo hapo. Ingawa ikiwa kuna shaka yeyote kwamba mwananchi fulani au nyumba fulani ile ya mwenyewe wameingia watu kule ambao tunafikiria kwamba ni wezi wameweka vitu vya kuibwa pale, hapo sheria ifuatwe tu akiingiliwa ni kwa kikananuni. Pia tunasema kwamba roho ya binadamu ni kitu ghali sana, kwa hivyo tumependekeza ile penalty au hukumu ya kuuwawa mtu tuiondoe maana roho ikitutakatifu na isichukuliwe na mtu yeyote, ikiwa kuna haja ya mtu kuathibiwa huwa ni kwa njia ya kuwekwa jela. Ni pendekezo huenda pengine wakatetea wakasema la roho ni kwa roho, eye for an eye and so on.

Kama nilivyosema disabled ni sehemu muhimu sana ya jamii yetu ya Kenya, tumewaekelea haki zao na wana haki ya kila aina ya uhuru kama wengine na kushiriki na uwezo wao kushiriki katika maisha ya kila siku kama wanavyoweza wao. Wapewe

nafasi kushiriki kufanya kazi maofisini, kufanya kazi katika idara za serikali, kufungua biashara kama wenzao, kupata mikopo kama wenzao ya kuweza kuendesha kazi zao na kadhalika. Haki ya kuheshimiwa, serikali ichukue hatua na kuweka sheria ya kuhakikisha kuwa shule tahasisi zote za walemavu yameunganishwa na maisha ya jamii kwa jumla. Isiwe yamewekwa kando ikaonekana ni watu wengine kabisa lazima njia zifuatwe au kanuni iwekwe na kila aina ya njia iwekwe ili kwamba wawe pamoja na sisi katika maisha yetu. Pia tusahilishe maisha yao, majengo marefu lazima yawe na lift ili mlemavu aweze kufika kule juu, wale ambao wapofu kati yao wawezeshwe kwa njia kwamba kila karatasi rasmi, kila taarifa rasmi ziandikwe kwa brail (ile njia maalum ili kuwezesha vipofu kati yetu wale wasioweza kuona waweza kufuatia vile inavyotendeka kwa njia ya kusoma, kwa njia ya brail na kadhalika).

Serikali iwezeshe walemavu kushiriki katika kila ustawi wa kukata shauri, yaani katika baraza za municipa katika idara tofauti tofauti, katika bunge wawemo walemavu kule pia. Na pia tumesema katika vyama vyama vya kisiasa, wakitoa ………… zao kama tutakavyowaeleza baadaye wasiwasahau walemavu. Tumekutana na walemavu wengi ambao wanahimu walemavu ambao wana uwezo wa kiakili kama tulivyosema moja wao, mimi na taabu ya miguu lakini sina tabu ya akili. Naweza kufanya kazi yoyote ambayo yote mwengine mwenye akili anaifanya na huenda nikamshinda pia, mara nipate nafasi niwekwe hapa kwenye baraza hili au lile na mtaona jinsi ambavyo mimi nitawatumikia wananchi. Kwa hivyo mlemavu afikiriwe uwezo wake na kila mmoja wao kati yao bila shaka ana uwezo fulani au mauliba fulani, ……… ambaye anaweza kuitumia na tunaweza kuitumia sisi wenzake wananchi ili tupate faida katika jamii yetu pale pale, katika idara basaran ya shule, parents associations, katika kusomesha, katika kuendesha skuli pia awe headmaster na kadhalika. Kwa hivyo tunasema kwamba tupendekeze walemavu washirikishwe katika maisha yetu ya kila siku na wapewe nafasi ya kufanya hivyo.

Kisha tunazungumzia haki za kidini kama nilivyosema kuna haki nyingi hapa zinahitajika. Haki ya kidini kila raia ana haki ya uhuru wa kidini, aweza kuabudu kufuatia dini ambayo anaifuata bila kuingiliwa. Pia awe anafikira za kidini bila kuambiwa fikira zako hizo ni mbaya au ni sawa sawa na maoni yake ya kidini. Muhimu ni kwamba hatukani dini ya mwengine akaleta mfurugano katika jamii, ila kutukanana dini hii kutukana dini nyingine hiyo ndio mipaka ya hati hii. Maana kila haki ina mipaka yake sio? Kwa hivyo hati hizi ambazo mtazisoma pia ina mipaka yake, mtu asiseme madhara vidi ya kabila fulani, maana ukianza kutukana kabila fulani itakuwa muingilia kabila nzima na wale pia watakutukana watu waanze kupigana. Kwa hivyo kwa upande wa dini tunasema kila raia ana haki ya kuabudu kufuatia mila au dini yake au kusoma au kusomesha dini yake, asizuiliwe na mtu yeyote kusoma juu ya dini yake au kusomesha dini yake. Na elimu ya dini tunasema itatolewa katika shule za serikali na kupewa kwa njia isiopendelea dini yeyote. Pia tunasema raia asinyimwe haki ya kuingia shule yeyote kwa ajili ya dini yake, na wewe huwezi kuingia shule hii maana dini yako ni dini fulani, hii shule ni ya dini fulani tu wewe huna haki ya kuingia. Tunazuia ubaguzi wa kidini kwa kila njia. Tutasoma kwa urefu zaidi juu ya mambo haya.

Tutaendelea mbele mtaona pia mfanyi kazi. Mfanyi kazi pia tunasema ana haki zake; ana haki yake ya kupata mshahara wa kutosha, mshahara uliomuadilifu (fair remuneration). Neno hili fair ilibidi tuitumie maanake hatuwezi kusema kila mfanyi kazi lazima apate shilingi fulani maanake kuna aina tofauti tofauti ya wafanyi kazi. Kwa hivyo tunasema kwamba apate mshahara

ambayo ni mshahara mwadilifu, ya kumtosha kuishi bila kujizalilisha na bila mashaka yeyote. Na hatukuwezi kusema mengi hapa maanake tumeambiwa na jamaa fulani kwamba hamkusema ya kutosha. Hii Katiba tumesema ndio kanuni kubwa, kanuni baba, chini ya kanuni baba kutakuwa na kanuni nyingi; kanuni mtoto, kanuni watoto au sheria toto. Kwa hivyo hatuwezi kusema kila neno katika katiba. Katika eneo hili la wafanyi kazi kutakuwa na industrial act, industrial relations act ambayo itaonyesha mahusiano kati ya tajiri na mfanyi kazi na hapo pia tunataraji kwamba mambo itakuwa ni ya uadilifu. Tuondoe mashtaka yaliyoko hivi sasa kwamba mfanyi kazi hapati pato la kutosha kufuatia kazi anayefanya, anastahili pesa nyingi zaidi lakini hapati na kuna malalamiko kwamba matajari wanawadhulumu wafanyi kazi. Kwa hivyo haya ni mambo ambayo yataweza kutengenezwa.

Tume pia imependekeza Tume kadha wa kadha kufanywa na kati ya Tume hizo kutakuwa na Tume inahusika na mishahara. Tume hiyo itahusika na mishahara ya kila mtu tangu rais mwenyewe mpaka mfanyi kazi wa ada na mawaziri wote na kadhalika na wabunge na bila shaka kutakuwa na njia nyingine ya kwamba mfanyi kazi hapa nchini atapata njia ya kwenda kulezwa juu ya mshahara wake na haki zake. Kwa hivyo ana haki ya mshahara muadilifu ana haki ya reasonable working conditions, hali ya kufanya kazi ambayo si mbaya, ambayo ni ya sawa. Asifanye kazi kwenye jua, tangu asubuhi mpaka jioni bila ya kupata kupumzika kwa mfano au anafanya kazi kwenye mtambo ambapo kila aina ya madawa mabaya au hewa mbaya inatoka na kumdhuru maisha yake. So working conditions ya mfanyi kazi lazima ziwe ni nzuri. To form, join or participate in the activities and progress of a trade union, kushiriki katika chama cha wafanyi kazi akitaka asizuiliwe kuwa mwanachama wa chama cha wafanyi kazi.

Pia awe na haki ya kugoma chini ya hali fulani, hivi sasa pia kuna mpango ambapo mfanyi kazi na matajiri wanakaa pamoja, wanazungumza, wasipopatana anakuja mtu kati yao, ministry of labour. Ikiwa hawajapatana basi mfanyi kazi asipotosheka huwa ana haya mgomo. Kwa hivyo haki hii ya kugoma kwa njia ya mwisho (last resort) tunasema kwamba apatiwe, asilazimishwe kuendelea kufanya kazi ikiwa mambo fulani ya haikutimizwa.

Pia katika haki hizi basic bill of rights, kama nilivyosema hiyo ndio ndefu kabisa katika sura zote hizi. Mtaona kwamba tumefikiria pia yule anayeshtakiwa, mshatakiwa. Mtu ameshikwa njiani bila sababu anatiwa kwenye gereza anasahauliwa huko au anapigwa, hapelekwi mbele ya korti. Yote haya tumezungumzia hapa. Tumesema kwamba lazima apelekwe before the court within 48 hours baada ya kushikwa na ikiwa atakuwemo ndani ya cell, asihadhibiwe, asidhalilishwe, asipigwe, apewe chakula chake, aweze kulala mpaka wakati atakapopelekwa mbele ya mahakama. Na pia tunasema ikiwa mbele ya mahakama hana mtu wa kumtetea, hana wakili wa kumtetea basi serikali impe wakili kumtetea, kuwe na public defender, mlinzi wa raia. Huyu atahakikisha kwamba huyu jamaa atasaidiwa kupata mtu kumtetea kwenye kesi wala hata kama amefanya jambo mbaya lakini alakal atapata mtu kumtetea, guilty or not guilty is another thing. Haya tumeyazungumzia kwa wingi sana ukurasa kumi.

Tukiendelea sura ya sita, ‘representation of the people’, uakilishaji wa raia na kama tujuavyo uakilishaji wa raia huwa katika

bunge au katika manusipa au city council na kadhalika. Na hapo hii maanake ni kwamba sasa katika sura hii tunazungumzia mambo ya uchaguzi, representation of the people. Tunasoma kwa urefu kule tumetaja mengi hapa, tumesema kwamba uchaguzi utakuwa kwa siri si mlolongo, kwamba uchaguzi utakuwa free and fair, uchuguzi huru na uadilifu na muadhilifu. Pia tunasema kwamba registration ya wananchi kupiga kura iwe continuous saa zote. Mtoto wangu leo amefika umri wa miaka kumi na nane anatakiwa afanyiwe registration aweze siku hiyo aende kwenye registration office aandikishwe awe ni voter au mpigaji wa kura. Pia tunasema kwamba chama chochote cha kisiasa kiwe na at least one third of the candidate for direct election should be women, theluthi moja ya wale ambao wataogomea uchaguzi katika party yeyote wawe ni kina mama. Candidates wawe ni one third. Baadaye tutazungumza zaidi juu ya kina mama.

The right to vote haki ya kupiga kura kama tulivyosema amri yeyote ambaye amefikia umri ya kumi na nane ana haki ya kupiga kura na amekuwa akikaa hapa kenya wakati huo. Pia tunasema kwamba lile sanduku la kuwekea kura liwe transparent wazi. Unaweza kuona kama glass, unaweza kuona ndani, kuna kitu hapo awali ama hakuna kitu. Tupu au si tupu saa zile za kuanza, the ballot boxes shall be transparent. Pia tunasema kwamba kura zihesabiwa pale pale zisipelekwe zisafirishwe kwengine, pale pale zihesabiwe na should be declared there and then.

Pia tunasema Electoral Commission ndio inaandikisha vyama vya kisiasa not the Registrar of societies. Registrar tunamuachia mambo zingine, welfare societies na mambo kama haya na NGOs na kadhalika, lakini Electoral Commission itashughulikia kusajili vyama vya kisiasa, pia ku-supervise, kusimamia sio General Elections pekee yake, presidential elections pekee yake. Pia vyama kisiasa huwa na uchaguzi wao wenyewe, huyu atakuwa chairman, huyu atakuwa treasurer, huyu atakuwa secretary general. Basi pia uchaguzi wa kila chama cha kisiasa pia utasimamiwa na Electoral Commission, tumewapa wanatume wa Election Commission hiyo kazi pia. Pia Electoral Commission itaendesha kazi ya kuelemisha wananchi kuwapa elimu ya raia juu ya mambo ya haki ya binadamu, haki ya raia, pia mambo yanahusu democracy, democrasia na kadhalika ili kwamba kazi hii ya kushtawisha hali kidemokrasia katika nchi, hali ya haki za binadamu, haki ya raia na kadhalika. Iwe mtu anainukia anajua haki zake. Kule america kwa mfano utamsimamisha mtu yeyote, atakuambia huwezi kunifanyia hivi chini ya Katiba fungu fulani fulani mimi nina haki ya kufanya hivi na hivi. Kwa hivyo elimu ya raia na kujielemisha haki zake raia ni muhimu sana, si leo tu tutapitia Katiba kesho tunaieka nyumbani tukaisahau.

Msome, muelemishwe, muhudhurie vikao vitakaofanywa katika kuelemisha wananchi au civic education. Hatukupendekeza kwamba elimu ya Katiba ifanywe katika curriculum na kadhalika wananchi wengi walipendekeza, lakini sasa inategemea pia minister of education na jinsi ambavyo curriculum zile au syllabus zitafanywa na tunaomba kwamba tumewahimiza wafikirie kwamba hisa fulani ya wakati katika shule ya watoto waelemishwe haki na pia uajibu wao wakiraia. You have to have your duties and you have your rights.

Tukiendelea tunasema kwamba pia kila chama cha kisiasa mbali na kuwa na kuwafikiria wakina mama na one third candidates wao wawe ni kina mama kwamba kila hesabu ya kila political party tutaisimamia, Electoral Commission itasimamia hesabu.

Kila chama cha kisiasa kitapeleka report juu ya kazi yake, wanachama walioko pesa gani walipata kutoka wanachama kwa upande wa subscription na kadhalika. Mnaitumia vipi pesa hizo maana hizo ni pesa za raia, sio? Kwa hivyo itabidi kutoa report juu ya kazi iliofanywa na pesa ulizonazo na wale ambao watatetea katika uchaguzi watakuwemo serikali itawapa pesa fulani sehemu fulani ya pesa kuwasaidia kuendesha kazi zao. Lakini pesa hizo tutazitumia kwa njia maalum sio kwa njia kwa mtu kutia petroli katika gari lake au mtu kwenda kujikalia kwenye hoteli la, ni katika kazi zile hasa la uchaguzi. Tunasema monies that is allocated to a registered political party from the fund of your sanduku shall be used only to cover the election expenses of the politica party and the broadcasting of the policies of the political party. Ikiwa KBC imechukuwa pesa kwa chama chochote, DP, NAK or whatever, wakitozoa pesa kule pesa hizo zinaweza kutoka kwenye hizo pesa za msaada ulizopata au for the organisation by the political party of civic education and the electoral processes. Ikiwa chama kitapokea pesa kutoka kwa serikali zitumiwe katika kuelemisha wananchi juu ya uchaguzi, kuelemisha wananchi juu ya demokrasia na kadhalika. Mtasoma kwa urefu zaidi juu ya mambo haya.

Kisha tunasema kila political party katika ile list yake ya candidates kugombea uchaguzi watakuwa na list alternate members. Ikiwa wa kwanza katika ile list ni mwanamume basi wa pili awe ni mwanamke, wa tatu mwanamume, wa nne mwanamke, wa tano atakuwa ni kijana (youth). Tungependa pia youth wapate nafasi ya kupelekwa kwenye bunge pia na kadhalika lakini kina mama wawe alternate between women and men in the priorities of the nomination. Na kila political party ile list yao ya wagombea iwe ni national outlook, wasiwe wote ni kabila moja ili kwamba kila political party iwe a national party – chama cha kitaifa, si chama cha kabila fulani. Tunaambiwa hivi sasa vyama vingi vya kisiasa kwa hakika vina msingi wa kikabila na wengi waliomo katika office bearers wale ni kabila moja na kadhalika.

Tukiendelea mbele basi tunafikiria structure of Parliament. Baada ya uchaguzi tunafikiria Parliament yenyewe na tunasema kwamba Parliament itakuwa na nyumba mbili si moja. Hivi sasa tuna nyumba moja, National Assembly. Sisi tunapendekeza kuwe na two chamber Parliament; National Assembly na National Council. National Council itakuwa na wajumbe mia moja, kila district itakuwa na mjumbe moja. Kwa hivyo itapata sabini kuchaguliwa hao. Kisha tutatia juu thelathini wengine kina mama na hao kina mama (wajumbe) thelathini, watachukuliwa kwa kila province wanne katika provinces saba, hao itakuwa ni ishirini na nane. Na wale wengine wa pili kuwafanya thelathini watakuwa ni wajumbe wa Nairobi, as a city as the Capital itakuwa na wajumbe wawili katika National Council. Hiyo ni nyumba moja. Nyumba ya pili itakuwa ni National Assembly kama hii ya sasa. Kama hii ya sasa itakuwa na wabunge mia mbili na kumi kama hivi sasa, kasha kutakuwa na wajumbe tisini wengine. Tumeambiwa kwamba kwa nini kuweka tisini ambao hawatachaguliwa, lakini kwa hakika ukifikiria jinsi ambavyo tutawachugua hawa utatambua kwamba tunaeneza au kustawisha udemokrasia kwa kuwatia ofisini. Vipi tutawachagua hawa? Hawa tisini watagawanywa kati ya vyama vyote vya kisiasa ambavyo vitakuwemo katika elections – KANU, NDP, KBC na kadhalika. Sasa wakiingia katika elections kila party si itapata idadi kadha ya kura, nchi nzima, kwa hivyo tutatizama katika kila party, party hii imepata kura milioni moja na mia moja, party ile million mbili na thelathini, party ya tatu million moja na nusu na kadhalika.

Kufuatia idadi ya kura zilizopata kila party itapewa sehemu fulani katika viti hivi tisini. Hii ni kama kutoa compensation maana tumesema hapa Magarini kumekuweko wachaguzi wawili, mmoja atamshinda mwenzake kwa kura tatu nne tu. Kwa hivi sasa maanake ni kwamba wale waliompigia kura yule mwengine aliyeshindwa kura zao zimepotea. Lakini tukizihesabu pamoja na kura za chama chao kisha tukawapa compensation viti kadha hivi ni kuwapa wale waliowapigia kura a sort of represention au uakilishi bungeni. Kwa hivyo tumesema hii ni system ambayo hutimiwa huko German hivi sasa. So 96 ni kama compensation kwa kila party inaitwa 'Least Member Proportional System (LMPS), inatumiwa katika nchi kadha. Hivi kwa hakika ni kama ni compensation na pia kustawisha udemokrasia katika nchi, yaani hatukuwasahau hata wale ambao wamewapigia kura wale waliopoteza seats au wale ambao hawakupata kuingia kwenye Parliament au kufaulu lakini kura zao zile hazikupotea. Kwa hivyo kila mmoja atahisi kwamba pia mimi nina mtu wangu pale ingawa kura zetu, kura yangu yule niliompigia kura hakupata lakini kwa jumla kura yangu na wenzangu katika party yangu tumepata viti fulani katika Parliament. Kwa hivyo National Assembly itakuwa na viti mia tatu, 210 plus 90. National Council hiyo nyumba mpya ambayo tunapendelea kuwekwa 100, ikiwa kati yao akina mama thelathini. Pia hapo National Assembly kutakuwemo kina mama pia maana tunasema katika ile list ya kugombea uchaguzi lazima wemo kina mama na wasiwekwe mwisho kwenye list wawekwe juum, one man one woman. Kwa hivyo bila shaka watakuwemo kila party, wakuwa wagombea uchaguzi ambao ni kina mama.

Sasa jambo muhimu sana ni kujua mamlaka kuna nyumba mbili, kazi ya National Council ni kitu gani, kazi ya National Assembly ni kitu gani. Hizi mbili pamoja National Assembly na National Council ndio itakuwa ni Parliament. Kwa hivi sasa ukisema National Assembly au Parliament ni sawa, maanake nyumba ni moja tu National Assembly. Weninge wanaita Parliament wengine wanaita National Assembly, lakini ikiwa na mbili pamoja, moja itaitwa National Council, moja itaitwa National Assembly, pamoja huwa ni Parliament. Kama Uingereza kule, Uingereza pia wana nyumba mbili, kuna nyumba House of Commons (nyumba ya raia), commons ni sisi raia na hawa wanachaguliwa. Kisha wana House of Lords (nyumba ya mabwana), siku zao Uingereza walikuwa na Lords na Peers, hao ambao walikuwa wakiimiliki ardhi hectares and hectares of land. Waliweza kupata mamlaka haya ya kuwa na nyumba yao pia wao kitambo sana kabla ya miaka nyingi sana, mia tatu mia mia tano hivi, lakini nyumba hizi mbili ndio zinaita Houses of Parliament or Parliament pamoja. Waamerica pia wana nyumba mbili – wana Senate na House of Representatives (nyumba ya waakilishi waliochaguliwa), pamoja inaitwa Congress.

Faida ya kuwa na nyumba mbili tumeona kwamba numba zote mbili zaweza kubuni sheria au kutoa mapendekezo juu ya sheria. National Council wajumbe walioko kule wanaweza kubuni sheria fulani, wakishapitisha sheria imepitishwa National Council itakwenda National Assembly na lazima ipitishwe kule kabla ya kupelekwa kwa Rais kutia sign iwe ni sheria. Kwa hivyo nyumba zote mbili ni sawa kwa njia hiyo, zote mbili zaweza kubuni sheria, kuanzisha ifanywe katika nchi, lakini National Assembly pekee yake ndio itakayoshughulikia mambo ya sheria inayohusu pesa. Sheria yeyote inayohusu pesa itabuniwa National Assembly pekee yake, National Councils hawezi kuzungumzia sheria inayohusu pesa. Hiyo ndio tofauti moja, lakini kisha wanagawanya kazi nyingine muhimu. Tumesema kwamba uchaguzi wa afisa yeyote mkubwa, uchaguzi wa vyeo vikuu baada ya Rais kuwachagua lazima ukubaliwe na bunge. Sasa hapa tumegawanya kazi hii ya ku-approve au kukubali appointments au uchaguzi wa watu, kwa mfano tunasema National Council ndio ambayo itapitisha uchaguzi wa wanatume

kadha wa kadha. Kwa hivyo wale ambao watachaguliwa kuwa Jucial Serve Commission, Tume ya kuchagua majaji, wanatume hawa lazima baada ya kuchaguliwa lazima wakubaliwe na approval from National Council. Pia National Council ita-approve wanatume wa National Land Commission, hii tume ndio ambaye sisi tunapendekeza iwe ndio itakayesimamia ardhi na mashamba na kuhakikisha kwamba mambo katika hali hii au eneo hili la viwanda mashamba na ardhi inaendelea vizuri na inachunguliwa vizuri sana.

Kisha National Environmental Management Commission (tume ya mazingara), Teachers Service Commission, Salaries and Remuneration Commission (tume ya kurekebisha mishahara), Constitution Commission (tume ya katiba). Hatusemi kwamba tume hii yetu itaendelea kwa muda mrefu, la, baada ya sisi kukamilisha kazi hii na kupitishwa na bunge watabaki watatu au watano kati yetu na kuendelea na kazi kuhakikisha kwamba mapendekezo yaliyomo katika Katiba yanatimizwa. Si kuwa tunafanya kazi tunawatupia shauri zenu la, haya ni mapendekezo kwetu yamepitishwa na Parliament lazima mtu afuatilie. Kwa mfano upande wa haki za binadamu, upande wa mazingara na kadhalika lazima kuweko mtu ambaye atasema hii tupendekeze jambo hili mbona halijafanywa mpaka sasa tafadhalini muanze kazi hii na kadhalika.

Pia National Council ita-confirm appointment ya Attorney General, Director of Public Prosecutions, Public Defender (mtetezi wa raia), tuliyemtaja yule ambaye atahakikisha kwamba raia atatetewa akipelekwa mahakamani ikiwa hana pesa ya kujitetea mwenyewe ya kumuweka wakili wake. Police Commissioner national council lazima ikubali kuchaguliwa kwake. Judges na Chief Kadhi pia National Council lazima iwakubali wale waliochaguliwa kuwa mahatimu na atakayechaguliwa kuwa Chief Kadhi. Hii kazi ya National Council.

National Assembly lazima ikubali Prime Minister maana katika serikali tumesema kwamba kuweko na Waziri Mkuu. Kwa hivyo National Assembly lazima imkubali yule baada ya rais kumchagua jina yake itakuwa mbele ya National Assembly iweze ku-vote huyu tumemkubali au huyu hatukumkubali na kadhalika. Deputy Prime Ministers watakuweko wawili, deputy ministers, permanent secretaries, mabalozi, Electoral Commission, wanatume wa Commission lazima wakubaliwe na National Assembly, Auditor General, Controller of Budget (yule atakaye-control mambo ya budget) Director of Central Bureau of Statistics na Governor wa Central Bank. Wote hawa baada ya kuchaguliwa National Assembly lazima iwakubali au ikiwa itawakata lazima wengine wachaguliwe. Mishahara ya wanabunge kama nilivyosema lazima iwekwe na hiyo Tume inayohusika na mishahara niliotaja sio wao wenyewe kujitengenezea mishahara yao. Kuna njia pale tumeeleza kwenye hii section ya Parliament.

Tukiendelea mbele tunaingilia chapter eight Executive. Kama ujuaavyo serikali ina sehemu tatu au sio? Sehemu moja ni Legislative ambayo tunazungumzia hivi sasa, hiyo inatunga sheria. Kisha kuna Executive, hiyo inayoweka sheria inatekeleza kazi ya sheria kama polisi, kama bwana DO hapa na wenzake na kumuanzia President mwenyewe of course na ministers. Kisha sehemu ya tatu ni mahakimu au Judiciary, tushamaliziana na Legislature. Sasa tunaingilia Executive. Executive ya tuseme nchi yetu kuna Rais mwenyewe kuna naibu wake Rais, kuna na cabinet mawaziri wengine na kadhalika, wote hawa wanaitwa

Executive. Sasa tukizungumzia utaona kwamba ukurasa wa tisa tunazungumzia authority of the President, mamlaka ya Rais. Hapa tunasema kwamba atakuwa ni mkuu wa nchi, mkuu wa dola, Head of State, atakuwa mkuu wa majeshi ya nchi, commander in chief of the defence forces, atakuwa mwenyekiti wa baraza ya amani ya nchi ambaye hivi sasa hatuna lakini tunapendekeza iweko. Pia Chairman of the Defense Council, baraza ya ulinzi wa nchi. Kwa hivyo Rais atakuwa ni mwenyekiti wa baraza hivyo vyote. Pia Rais ana kazi muhimu ya kuwa ni ishara ya umoja wa nchi, si lazima aweko mtu mmoja tu ambaye ni symbo, ishara au kinara cha umoja wa wananchi. Kwa hivyo kazi yake ni muhimu sana na yeye ana jukumu ya kuendelesha na pia kustawisha umoja wa nchi yetu, kuhifadhi sovereignty wa nchi yetu, siada ya nchi yetu ili kwamba tusiingiliwe na nchi yoyote ingine. Pia atakuwa ni mwenye ku-promote kustawisha na pia kuheshimu watu wa nchi yetu wakiwa ni makabila tofauti tofauti na pia atasaidia katika kuhami au kulinda haki za kibinadamu na haki za kimsingi (fundamental freedoms). Hiyo moja ni kazi kubwa ya Rais.

Rais pia shall uphold, safegaurd and respect the constitution and the rule of law. Pia Rais ndiye atakayelinda Katiba yetu na ambaye ataheshimu Katiba yenyewe na pia ataheshima kanuni/sheria ua utawala na Rais ataendesha mamlaka yake kufuatia Katiba hii ya Kenya. Pia Rais asiwe na ofisi yeyote au kazi yeyote ingine ila hii ya urais na asiwe kwenye party yeyote au chama cha kisiasa chochote chingine. Hii ni kuhakikisha kwamba yeye ni baba wa taifa nzima, baba ya kila mwananchi na hapendelei chama hiki cha kisiasa au kile. Hata kama ametoka kwenye chama fulani akiwa amechaguliwa kuwa Rais awache kazi yeyote kuhusu kile chama ambacho yeye alikuwa ni mwanachama wake. Hizo ndizo kazi zake. Pia tunasema Rais atafungua bunge, aweze kuwa na kikao chochote maalum au mahususi ya bunge, anaweza ku-address bunge wakati wowote atakayo na ata-dissolve Parliament, ataivunja bunge katika hali maalum tu. Hali hiyo ni ipi? Hali ya kumchagua Waziri Mkuu. Akimchagua Waziri Mkuu jina hilo la Waziri Mkuu atakuwa ni yule kiongozi wa chama kilichopata kura nyingi zaidi katika bunge. Yule kiongozi wa chama hicho ndio atakayechaguliwa na Rais kuwa ni Waziri Mkuu, lakini sasa jina lake lazima lipelekwe Parliament ndio imkubali kuwa Waziri Mkuu.

Parliament isipomkubali Waziri Mkuu, Rais atamchagua mwengine ambaye anafikiri huyu atapata kupigiwa kura kwenye Parliament na kukubaliwa. Huyu wa pili asipokubaliwa Rais ataivunja Parliament na ataamrisha uchaguzi mpya ufanywe na kisha ata-repeat, atapitia njia hiyo hiyo kupitiwa na Parliament mpya yule mwenye kuongoza kile chama ambacho kimepata kura zaidi na idadi kubwa ya viti ataitwa awe ni Waziri Mkuu. Mmefahamu nafikiri. Na katika hali hiyo hiyo pekee yake tu, hali ya kutoweza kupata mapatano au kuwafikiana na Parliament kumkubali yule waziri mkuu katika hali hiyo tu ndio Rais anaweza kuvunja bunge ili mwingine aingie ajarabu kuunda serikali. Lakini mtasoma zaidi.

Ni nani anaweza kuwa Rais? The person who is qualified as a presidential candidate is the citizen of Kenya by birth. Ikiwa ni mwananchi wa kenya kwa kuzaliwa huyu anaweza kusimama kuwa Rais. Pia awe amefika umri wa miaka thelathini na tano na kitu lakini asiwe zaidi ya miaka sabini. Hapa pia tumesema kwamba sharti hii ya umri kwamba isiwe zaidi ya miaka sabini haitawafikana na uchaguzi utakaokuja hivi sasa. Sharti hii itatumiwa katika uchaguzi utakaofuata, si uchaguzi utakaokuja hivi sasa. Kwa hivyo wale ambao watapigania kiti cha urais, ikiwa umri wao zaidi ya sabini wanaweza kuingia katika uchaguzi huu

ujao, lakini uchaguzi utakaofwata lazima awe mtu chini ya miaka sabini ili akubaliwe kugombea kiti cha urais. Pia awe ni mtu mwenye tabia njema, hana doa lolote, au aibu yeyote, awe ana degree (holder of a degree), shahada ya degree kutoka chuo kikuu ambacho kinatambulikana kuwa ni maarufu, chuo kikuu kinachojulikana. Awe nominated by a registered political party, huyu ndio ana-qualify.

Tukiendelea mbele maana kuna mengi na wakati unakwenda haraka zaidi ambavyo ningependa. Pia kama nilivyosema kuna uwezekano wa kumuondoa Rais pia, tumeeleza hapo na Rais anaweza kuondolewa kwa sababu kadha. Anaondolewa ikiwa inajulikana kwamba huyu hawezi kuendesha ile kazi au ni mgonjwa, ana ugonjwa wa kimwili au ugonjwa wa kiakili. Lakini kabla ya kuondolewa lazima achunguliwe kuwe na kamati ya madaktari kumpima na kamati hiyo itapeleka report yake mbele ya Parliament. Ikiwa imependekeza aondolewe Parliament lazima ipige kura, National Assembly na two thirds, suluti mbili ikipitisha kwamba aondolewe, Rais ataondolewa. Pia Rais anaweza kuondolewa kwa njia ya pili ikiwa matalan amefanya jambo mbaya sana (gross misconduct) au amevunja Katiba rais anaweza kuondelewa. Ikiwa imethibitishwa kwamba Rais amevunja yeyote Katiba ambaye itapitishwa mwishowe na kuna dalili kuwa amefanya hivyo, kufuatia pia uchunguzi wa kamati maalum itakayowekwa basi Rais anaweza kuondolewa. Au gross misconduct, kitendo kibaya sana ndio pia anaweza kuondolewa. Na Rais anaweza kujitetea mbele ya hiyo kamati sikufanya hivyo hakuna ushahidi na anathibitisha kwamba hakufanya hivyo basi kamati itasema hapa hakuna msingi wa kumuondoa Rais. Lakini uwezekano uko katika hali nilizozitaja.

Kisha Prime Minister nimeeleza jinsi ambavyo atachaguliwa, yeye ndiye atakayekuwa ni mkuu wa serikali (head of government), atakuwa na makamu wake wawili Deputy Prime Ministers, atakuwa na Ministers na ministers watachaguliwa katika nje ya bunge. Hawatakuwa wabunge na assistant ministers pia kutoka nje ya bunge. Deputy Prime Minister watakuwa wabunge wawili, so Waziri Mkuu na makamu wake wawili watakuwa ni wabunge, lakini ministers na assistant ministers watachaguliwa kutoka nje ya bunge kati ya raia na uwezo wao ule na kwa nini wamechaguliwa. Lazima Prime Minister aelezwe kwa nini amewachagua wale wala hakuwachagua wengine na lazima bunge ipitishe majina yao kabla kuwa mawaziri. Maelezo yamo kwenye mswaada, mtasoma wenyewe.

Kisha tukiendelea tuna chapter nine, kwa sura ya tisa ambayo inahusika na ile sehemu ya tatu ya serikali, sehemu ya mahatimu. Hapa badiliko moja tuliofanya tumeongoza aina ya korti. Tumesema kuweko pia na Supreme Court, hivi sasa tuna appeal court sio court of appeal. Kuna Sub-ordinate Courts, Magistrate Courts, High Court, Court of Appeal, mwisho ni hapo. Ndio kwa maana kuwa kuna Supreme Court ya juu kabisa, kwa mfano mambo makubwa tuseme kuhusu Katiba kuvunjwa au haikuvujwa au jambo hili je linagongana na Katiba au la tumeona kwamba kuwe na korti maalum kufikira mambo hayo makubwa zaidi. Na mkuu wa mahakama hiyo atakuwa ni Chief Justice. Pia mabadiliko tuliopia leta ni katika Sub-ordinate Courts, Magistrate Courts tunazo, tumependekeza tribunals, korti za kienyeji nazo ziwe nyingi zaidi. Pia tumesema kwamba korti za Kadhi, wandugu zetu wa Kiislamu kuwe na korti za Kadhi thelathini at least, lakini itategemea jinsi nchi ambavyo itaendelea na ikiwa kuna sehemu fulani hazipati utumishi wa korti ya Kadhi basi labda idadi ya korti ya Kadhi ama koti ya Kadhi itaweza kuzidishwa pia.

Pia tumesema jinsi ambavyo Kesi itasikizwa kwenye korti ya Kadhi, ifikie wale ambao walileta kesi hiyo mbele yake au hawakutosheka wanaweza kuendelea mbele. Kutakuwa na Kadhi's Appeal Court or Court of Appeal, ikiwa hawatatosheka hapo wataendelea mbele zaidi. Appeal Court ya Kadhi itakuwa ni Chief Kadhi na wenzake wawili, Senior Kadhis ndio watakaosikiza na korti hizo hazitaingiliwa na sheria yeyote ila sheria ya Kiislamu ndio itayofutwa katika korti hizi za Kadhi. Hivi sasa utaona kwamba mtu asipotesheka na hukumu ya Kadhi hata mimi nitakwenda High Court na huku utanona kwamba wanafwata sheria ambayo si ya Kiislamu. Kwa hivyo waislamu wamelalamika sana kwamba ingawa ni Waislamu hali ya kibinafsi ile kuhusu mirathi, kuhusu ndoa na talaka inaingiliwa na mtu ambaye na anatumia sheria ambayo si ya Kiislamu. Kwa hivyo sasa tunaona kwamba mambo haya yote ambayo inamhusu mwislamu yasikizwe na shauri ikatwe na hukumu ikatwe na Makadhi wakiislamu. Na pia tunaeleza jinsi ambavyo Kadhi wanaweza kuchaguliwa. Tunasema kwamba Kadhi atachaguliwa na Judicial Service Commission, ile Tume ya mahakimu, mahala ambapo Majaji wote pia wanachaguliwa na Tume hiyo. Basi pia Makadhi watachaguliwa na Tume hiyo hiyo. Katika Tume hiyo Chief Kadhi atakuwa ni mwanachama pamoja na mwanamke mmoja wa Kiislamu pia atakuwa ni mwanachama hiyo ya Judicial Service Commission.

Tunasema pia Chief Kadhi lazima awe na qualifications fulani, isiwe anachaguliwa na mtu hujui ni nani aliyemchagua au vipi, lazima awe ni mtu ambaye ni Mwislamu ambaye umri wake haupungui miaka thelathini na tano. Pia awe na shahada ya kuwa Wakili (an advocate), awe ni wakili wa High Court kama Majaji wengine. Na awe na experience, muda wa kuhudumu wa kutumikia watu kwa muda wa miaka kumi kabla hajachaguliwa kuwa ni Chief Kadhi. Kadhi na Senior Kadhi awe ana qualifications, advocate of the High Court lakini experience ya miaka mitano tu. Hayo ndio mabadiliko ambayo tumeyapendekeza katika eneo hili la Sheria au Judiciary.

Kisha tumeingilia mambo ya devolution of power – jambo muhimu sana – mgawanyo wa mamlaka. Mamlaka ni kile kitu power, yule mwenye power nyingi ndiye anaweza kuitumia atakavyo yeye. Lakini tumeona kwamba wananchi kila tunapokwenda wamesema kwamba wanataka mamlaka igawanywe, asiwepo mtu mmoja tu mwenye mamlaka nyingi sana kufanya atakavyo yeye. Pia watu walishtaki kwamba hawapati utumishi nzuri katika maeneo yao maana mambo yote yanafanywa Nairobi tu. Sisi hapa hatuna mwenye kututumikia na mtu wetu huko Nairobi Mbunge wetu hatumuoni mara nyingi, kwa hivyo tungependelea serikali ije karibu zaidi na wananchi na mamlaka pia yenyewe ikuje karibu zaidi na wanainchi. Watu wamependekeza kwa mfano kwamba hapa Pwani na kule Rift Valley tuwe na majimbo. Sisi tumependekeza aina fulani ya majimbo lakini asasi au msingi wetu si jimbo nzima bali ni wilaya, tumeipa kila wilaya mamlaka. Kwa hivyo nchi nzima tumegawanya na katika kila sehemu tumeweka watu pale kuwatumikia wananchi. Tumeanza vijijini, tukapendekeza kwamba kila kijiji kiwe na baraza lake. Kila kijiji kitakuwa na baraza na wanachama wa baraza hiyo ama watachaguliwa na wananchi au watapigiwa kura na wananchi na kupendelea wawe ni wazee wa vijiji. Lakini wananchi wanahaki pia ikiwa hawapendelei wale wazee wao katika eneo lile maana nchi ni kubwa. Pahala pengi ambapo tumekwenda watu walipendelea kwamba elders (wazee) wapewe mamlaka zaidi, maanake wanawapende wanasema hawa ndio wako karibu na sisi sana na wanatutumikia zaidi ya Provincial Administration, zaidi ya DO mwenyewe au zaidi ya chief. Kwa hivyo tunataka wazee wetu wapewe

mamlaka na pia walipwe kitu fulani kwa kazi zao ambazo wanazifanya. Kwa hivyo tumesema kwamba kila kijiji liwe na baraza, baraza linawezakuwa ni wale waliochaguliwa au waliopigiwa kura. Watakuwa kiasi cha wazee sita hivi kwa kila kijiji.

Kisha juu ya kijiji tuko kwenye Lcation Council, kuwe na baraza la location pia. Na baraza hilo la location liwe ni wanachama wake wawe ni wajumbe katika vijiji, kila kijiji kitapeleka mjumbe wake kwenye location na kuzungumzia mambo ya location sasa. Baada ya kuzungumzia mambo ya kijiji, sisi kijiji chetu kina shida fulani, watazungumzia shida za kijiji katika Location Council katika higher level. Mbele zaidi tunasema kwamba kuweko na serikali ya wilaya na hapa kwenye serikali ya wilaya ndipo ambapo tumeweka mamlaka ya kutosha. Mamlaka ambayo wengi kati yenu labda mmependekeza iwe katika baraza la jimbo or regional assembly, tumetia mamlaka hayo katika serikali ya wilaya. Nitawaeleza ni mamlaka gani ambayo tumeipa serikali ya wilaya. Kwa njia hii tumesema kwamba mkaaji wa wilaya hiyo haitamlazimu kwenda mbali sana kupata utumishi. Na tunasema kwamba baraza hii litakuwa pia ni watu ambao watapigiwa kura na wananchi, hawatachaguliwa. Kila Wilaya itakuwa na uchaguzi wake wa kupiga kura na wote watakaopelekwa kwenye baraza hiyo ni wale ambao wamepigiwa kura na mkuu wa Serikali hiyo ya Wilaya ataitwa District Administrator. Wanachama wa baraza hiyo ya wilaya idadi yao itakuwa kati ya ishirini na thelathini.

Sasa ni madaraka gani ambayo imepewa baraza hiyo ya wilaya? Mkitizama katika ukurasa wa 45, tuna list ya mamlaka ya serikali ya kati (Central Government), na chini yake kuna list ya mamlaka ya District Government. Tunasema kwamba serikali ya kati itahusika na ulinzi, mnaiona pale juu National Defense and Security? Wengine mshaiona, ukurasa 45 ya Daily Nation. Kwa hivyo Serikali ya Kati (Central Government) itahusika na mambo ya ulinzi wa nchi, itahusika na mambo ya mahusiano kati yetu na nchi zingine au international relations, itahusika na international trade, itahusika na sarafu, itahusika na planning ya ustawi, mipango ya ustawi katika nchi nzima, itahusika na uchaguzi katika nchi nzima, itahusika na national resources (mali ya asili ya nchi) na kadhalika. Lakini muhimu zaidi kwetu kwa wale hasa ambao wangependa kupata serikali karibu na nafasi yao ni ile list ya pili ambayo inaanza ukurasa 45 chini kabisa. Inasema kwamba, “government implementation or development plans”, serikali ya wilaya ita-implement itafanyia kazi mipango ya ustawi katika wilaya. Pia serikali ya wilaya itahusika na kufanya kodi katika eneo lile ya wilaya na kodi hiyo itatumika pale pale wilaya. Pia itahusika na elimu, huduma au utumishi wa elimu kuwapatia wananchi katika wilaya hiyo elimu. Elimu itakuwa ni ya nursery, primary na secondary, hiyo itakuwa ni kazi ya district government. Pia medical and health services, matibabu katika wilaya hiyo itakuwa ni jukumu na mamlaka ya district government. Pia water services, kuwapa wananchi maji, kujenga barabara (road services), markets and trading centres, soko zote na maeneo ya biashara na kadhalika au vituo vya biashara.

Serikali ya wilaya pia itahusika na mipango yote katika wilaya hiyo. Pia huduma za ukulima itasimamiwa na serikali ya wilaya. Pia huduma za ukulima zitasimamiwa na serikali ya wilaya. Probation and welfare, community development, cultural affairs, mambo inayohusu utamaduni na kadhalika. Kwa hivyo mtaona kwamba kila wilaya itakuwa na serikali itakayoisimamia hudum zote au kila aina ya utumishi ambayo watu walikuwa wakilalamika kwamba mambo haya hatufanyiwi kwa kuwa serikali iko mbali na sisi. Kwa hivyo serikali yao ya wilaya pale wilaya ndio atakuwa na jukumu ya kuendesha kazi haya. Kama ambavyo

wengine walitaka majimbo. Jimbo ni kubwa kuliko wilaya, lakini sasa tumeileta serikali karibu zaidi. Kwa hivyo Malindi district hamna haja kwenda mbali kufuatia au kupeleka mashtaka yenu, tuko na Malindi Town. Pia mtakuwa na wajumbe wenu ambao mtawaendea mkawaambia, “mbona baraza lenyu halikufikiria jambo hili au jambo lile, hatuna taa katika eneo hili usiku tunashambuliwa na magaidi na kadhalika”. Kwa hivyo serikali imeletwa karibu zaidi kuliko serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo ingekuwa iko Mombasa kwa jimbo la Coast na ni mbali kwa wengine, watu wa Lamu lazima waende kule. Lakini sasa tumeleta serikali kwenye wilaya yenyewe karibu zaidi kwa kila mwananchi na tumeanzia kule kwenye kijiji. Kuna mengi ambao mtasoma wenyewe.

Kuwatuliza moyo kidogo, kuna wilaya zingine ambazo zina mali ya asili ya kutosha, lakini zingine hapa nchini hazina, maskini sana. Kwa hivyo ni wajibu wa serikali pia kutoa hisa fulani kwa kila district kuongeza pesa kufuatia idadi ya raia wanaokaa katika wilaya hiyo ikiwa ni wengi sana, kwa hivyo kodi au pesa ambazo ni msaada ya serikali ya kati ya Nairobi itakuwa ni zaidi kwa district ambayo ni maskini kuliko district ambayo haina matatizo makubwa sana. Kwa hivyo kutakuwa na uadilifu na pia tumeweka Tume maalum kuhakikisha jambo hilo, Tume ambayo ni council au baraza (Economic and Social Council) ni muhimu sana hiyo. Kazi yake kati ya kazi nyingi sana ambazo council hii itafanya ni kuwa saa zote ina uangalifu, katika eneo fulani hawa hawajajengea barabara za kutosha. Tumefanya uchunguzi tukaona kwamba mapato yao ni kidogo sana hata ingekuwa wanataka kujenga barabara hawawezi. Kwa hivyo watawaambia serikali ya kati ya Central government, “hawa wanahitaji pesa nyingi zaidi, mtawapa pesa nyingi zaidi ili watimize mipango yao ya usawi na kadhalika”. Na mengi zaidi ambayo ningependa muyasome hapo maanake sina time na naazimia kumaliza hapo saa sita lakini tafadhalini mtanipa dakika tano kumi hivi kumalizia jambo la mwisho ambalo ni jambo la mashamba na ardhi. Hiyo ni sura ambayo pia ni muhimu na bila shaka mngependa kujua yale tuliopendekeza hapa.

Mambo ya ardhi ni muhimu sana na kila tulikokwenda wananchi walilalamika sana juu ya jambo kama hili kwa njia mbali mbali. Wale waliosema kwamba wengine wana ardhi maelfu ya acre na wengine hawana chochote hata nusu ya acre ua robo ya acre au kwamba ardhi inatolewa kwa njia ambayo sio ya haki na kadhalika. Na wale ambao wanasema tumekuwa tukiishi kwenye eneo hili kwa muda mrefu sana lakini mpaka leo hatuna title deed na kadhalika. Kwa hivyo tumesema kwamba tatizo hili la ardhi lazima lichunguliwe na kwa muda kati ya miaka miwili mambo haya yatazamiwe, yastawishwe au yatatuliwe. Tumesema kwamba katika muda huu tumeipa serikali miaka miwili kuchungulia mambo haya. Katika muda wa huo miaka miwili, tunasema kwamba kuwekwe njia za kuchungua na kupata makisio ya malalamiko ya wananchi. Malalamiko ni mengi, malalamiko haya yana msingi gani na tukishafanya hivyo hasa katika maeneo ya Pwani, Kaskazini Mashariki na Rift Valley maana malalamiko ni mengi sana katika mikoa hii mitatu. Kwa hivyo tunaitaka serikali, tumeipa muda serikali miaka miwili baada Katiba hii kupitishwa kuwa ni Katiba yetu kirasmi wafanye uchunguzi ili kujua kwa hakika malalamiko haya yana msingi au la.

Pia tunasema kwamba katika muda huu wa miaka miwili serikali itafanya uchunguzi katika mashamba na ardhi zilizotolewa ili kuhakikisha ikiwa zimetolewa kwa njia za kisheria au la. Tunaambiwa about land grabbing, tunasema kwamba hii land grabbing kupura ardhi na mashamba pia katika muda wa miaka miwili serikali ifanye uchunguzi na ikiwa kuna mikono ambayo imepura

arthi bila ya hati, basi mashamba hayo yachukuliwe na serikali irudi katika mikono ya serikali na kisha itolewe kuwapa wale ambao wanahaja ya ardhi hizo. Pia tunasema kwamba katika muda wa miaka miwili baada ya Katiba hii kupitishwa kwa rasmi, bunge itapitisha sheria kushtawisha kanuni zote zinazohusu ardhi. Kwa hivi sasa tumeambiwa na watu wengi wanaohusika na ardhi kwamba kanuni zinazohusika na ardhi ni nyingi sana na ni complex, zinagongana hapa na pale. Kwa hivyo kuna haja ya kushtawisha kanuni hizi ziwe ni wazi zaidi na rahisi zaidi na tumesema kwamba kuwe na Tume ya ardhi itakayochungulia mambo haya.

Pia katika muda huu wa miaka miwili wale wanaitwa ma-squatter, tumepata mashtaka mengi kwamba wananchi wengi wanaishi kama ma-squatter. Wanaitwa ma-squatter maanake wakati wowote wanaweza kuondolewa hapo walioko na tunasema kwamba katika muda huu wa miaka miwili ma-squatter wote wapewe makao, yaani tutatue kabisa na kwa njia ya mwisho kabisa tatizo hilo la ma-squatter hapa nchini. Pia tunasema kwamba mtu asiyekuwa raia asiwe na haki yeyote ya kumiliki ardhi hapa Kenya, raia amuuzie mkenya ikiwa ni ………… na pia tunasema kwamba asiyekuwa raia (non-citizens), waweza kupata ardhi kwa leasehold pekee yake, isiwe ni freehold. Leasehole utampa mtu asiye raia atumie kisha arudishie serikali na pia leasehold isizidi miaka tisini na tisa. Kuna maeneo ingine ambapo lease ni miaka mia tisa na tisini na tisa na vizazi vingapi vitakufa kati ya leo na hapo ambapo ardhi hiyo itarudi kwa serikali. Kwa hivyo tumepunguza leasehold kufikia miaka tisini na tisa. Kwa hakika ni mapendekezo hayo tu ambayo tumeyatoa kuhusu ardhi. Pia tukumbuke kwamba kuna Tume nyingine ya Njonjo ambayo imechukua wakati mrefu katika kuzunguka na kusikiza maoni ya watu na malalamiko yao juu ya ardhi. Tume hiyo ya Njonjo haijatoa maoni yake na tuombe kwamba ikitoa maoni yake na ripoti yake, ikilinganishwa na kuwekwa pamoja na hii Katiba mambo itastawishwa katika eneo hili muhimu la ardhi.

Kuna mengi mengine ya kusemwa lakini wakati ndio mrefu lazima tumalize saa saba, tumepewa saa tatu. Nimekuwa nikizungumza sasa ni saa mbili tangu kuanza. Kwa hivyo ningependa saa hii ya mwisho tutumie katika kupata swala zenu au fikira zenu au maoni yenu juu ya hii Katiba tuliopendekeza iwe ndio Katiba yetu mpya. Asanteni kwa kunisikiza na poleni nimeendelea kwa muda mrefu, lakini ninafikiri mtafahamu kwa nini nimefanya hivyo. Asanteni.

Mwenye swali atakuja atatupatia jina lake halafu atauliza swali lake. Kwa hivyo wenye swali nitawapatia namba mtakuja karibu. Number one, number two, number three mpaka number ten, tumalize na hawa kwanza. Mje karibu mliopatiwa number nyote.

**Samuel Kimaiyo arap Serem:** Asante sana Prof. Idha kwa kututemblea leo mara ya pili. Swali langu ningependa kuuliza ni kuhusu upande ambapo nimesikia kwamba wale mawaziri hawatateuliwa kule bunge ama kama wabunge. Je, hawa watateuliwa kivipi kwa sababu hapo sikupata sawa sawa. Swali la pili, je katika mambo inaohusikana na mambo ya raslimali kama hapa tulipo wakati huu raslimali ambapo tukonazo ni aina mbali mbali lakini katika hizi rasilimali kuna zile ambazo zingelichangia zaidi katika government revenue ambapo hizo ndio moja wapo ndipo tutakwenda kwa mambo ya regional government. Na ya tatu ni kwamba upande wa kazi. Tumeelezewa kwamba serikali itaulizwa ili iangalie mambo ya kazi, je

kama upande wa kazi mmesema kwamba itahusiana na mambo ya maadili ya ile kazi jinsi inaweza fanywa. Katika production ya ile kazi, kama ni kazi ya kuchimba madini na pengine kupasua mbao, je kutakuwa na tofauti ya ajira. Kama kuna mambo ya mineral resources, kama vile hapa kuna mambo ya chumvi, vipimwe je kwa tani ama vipimwe kwa futi kama vile inavyopimwa. Hapo ninafikiri pia ingekuwa bora zaidi. Ya tatu ni kama mazingara. Tuna mazingara pale kazi inapofanyika, kuna mambo tofauti, watu pengine wanazidi kukanyaga chumvi na miguu yao inabidi kuhudhuriwa. Kwa mambo kama yale ndio tungetaka tusikie tukiambiwa. Sio mambo ya Katiba pengine kwa maofisi kule juu, kubadilisha mambo ya president na hivi na hivi, lakini zile immediate problems ambazo tukunazo wenyewe hapa. Kwa hivyo hayo ndio nilikuwa nayo.

**Joseph Karayu:** Kwa jina naitwa Joseph Karayu. Asante sana Prof. Idha kwa kututembelea. Ninayo swali ya kuhusiana na wafanyaji kazi. Pale ulizungumza kwamba vijana wengi watoto wanauza barafu na nini, ni kwa sababu ya umasikini. Tunapenda katika Katiba hii mpya ni kwamba wafanyaji kazi wa kila jimbo kuanzia juu mpaka chini wawe ni wafanyaji kazi wa jimbo hilo hilo pekee yake. Kama kwa mfano pwani, unakuta kazi zote za ofisi za serikali, unakuta ni wageni katika bara na wakati huu ndio ambavyo inavyoendelea. Katiba mpya tunavyotaka ni kwamba mwende mkarekebishe wafanyaji kazi kuanzia juu mpaka chini hata anayefagia awe ni mfanyaji kazi wa jimbo hili pekee yake. Hapo ndio itafanya kupunguza ule umasikini watoto kutouza njugu karanga na kupunguza akina mama kuuza kuni ndio wapate unga, na kupunguza vijana watoto wadogo kuenda kuvunja chumvi.

Pili, katika hali ya rasilimali ya kila jimbo inapofanywa kazi, kwa jimbo lile inatakikana wapate commission ya juu zaidi kuliko zile pesa kuchukuliwa kwenda majimbo yale mengine. Tatu; katika ulinzi hatuna ulinzi ya kutosha kama vile tumewaelezea pengine hapo nyuma, ni kwamba vijana askari wote watakaoajiriwa kutoka vijijini, kila mji kuwe na askari ambao watalinda ulinzi maanake mgeni wowote akiingia watajua huyu anatoka wapi na lengo lake ni nini ndio hali wananchi wataishi katika hali ya usalama. Ni hayo tu.

**Stephen Kombe:** Kwa majina naitwa Stephen Kombe Kirumo. Mimi kwa mapendekezo yangu ni kuhusu mambo ya president. Ikiwa katika nchi yetu wanategemea wananchi kuwa ndio wenye mamlaka zaidi, kwa nini president wa Kenya hangeweza kuchaguliwa na wananchi wenyewe. Pili ni kwamba upande wa hali wa binadamu tunapita upande wa hali ya kimaji. Mwadamu wowote hapa katika Kenya yetu hii nguvu yake ni maji. Watoto hapa hawawezi kusoma bila maji, kitu chochote hapa hakiwezi kufanyika bila maji. Kwa nini maji yasiwekwe upande wa Katiba katika mstari wa kwanza. Upande mwengine, tukiangalia katika upande wa kikazi wafanyaji kazi wa company za chumvi. Utakuta wananchi wengi sana wanapata taabu sana. Mwananchi anatoka nyumbani anatoka na karai anateremka kule chini, anaende kuingiliana na zaidi ya tani tano akibeba chumvi apeleke nje akiwa amebeba na kichwa na mshahara wake huyo mwananchi analipwa shilingi mia moja ama shilingi mia tatu wanagawanya watatu kwa kubebana na chumvi iliyo nzito zaidi. Hiyo tunaomba kama inawezekana watu wa makampuni za machumvi watimize vizuri kwa upande wa wananchi, wanaumiza wananchi zaidi. Iwekwe katika Katiba hiyo.

Kitu kingine ambacho kile wananchi kinatusumbua katika roho zetu, ikiwa basi viongozi ambao wanatoka katika nchi yetu

kama Magarini Division, tunawachagua wenyewe ndio waende katika Parliament. Kwa nini basi wakiwa wameenda kutuchukulia ujumbe kule wakiwa wameweka mkutano wao hawaturuhusu sisi wananchi wenyewe waweze kupata mawaidha kutoka kwetu katika mkutano wao. Hiyo tunaiomba kama inawezekana kwa sababu mbunge anapoingia katika ……….(inaudible) huwa amepokea ripoti kutoka kwa wananchi, kule mbunge anaenda na ripoti gani kama hakuonana na wananchi. Kwa hivyo tunaomba hapo tuwekwe katika mstari wa mbele katika Katiba hii mpya wajue sisi tunatambulika na sisi ndio wenye kura kuwapigia nyinyi ambao mnaenda kwenye Parliament. Asanteni sana.

**Emmanuel Masha:** Kwa jina ni Emmanuel Masha. Bwana Professor tunakushukuru kwa kufika hapa siku ya leo. Kitu ambacho nataka kuchangia ni juu ya hizi mali za asili ambazo kwamba tunazo hapa kwetu. Hizi mali za asili utakuta kwamba kuna watu wanakuja investors wanakuja kufanya kazi hapa, lakini unapata kwamba kiwango fulani cha pesa ambacho kwamba hubaki ama hutolewa kwa kufaidisha community ama wakazi wa sehemu unakuta pesa zile zinapotea kiasi cha kwamba hata kule zinakwenda hazijulikani. Maoni yangu mimi ningeomba kwamba kuna mali za asili ambazo kwamba zinatolewa makodi, kama vile mikoko. Vile kama msitu umefungwa na miti haitolewi kule na ni mwananchi ambaye kwamba ni wa kawaida ambaye kwamba hawezi kujenga na mawe anatumia miti na inambidi atoe pesa apate permit ya kukatia miti na ile miti ambaye kwamba inaweza kumfaidisha. Ningeomba kama ingewezekana ile Katiba kwa mjengaji wa kawaida anajenga kwa boma lake akate mti tu kama mti ambao imetoka sehemu yake imfaidishe yeye mwenyewe. Isipokuwa basi wale wanatoka sehemu za nje wakija kuchukua miti na gari wakienda kule wawe wanatozoa kiasi fulani kwa sababu wawache ile ada hapa ifaidishe watu wa hapa. Itakuwa ni vibaya mimi natoka hapa ninunue mti hapa nijijengee hapa, lakini itakuwa ni vizuri kama ni gari imekuja inasongeza mti inapeleka kule lakini kuwe kuna commission ya fedha ambazo zinawachwa pale mahali ya kufaidisha community.

Sehemu ingine ni sehemu ya elimu. Kama vile nimesikia elimu ya msingi iwe ni bure, basi kwa maoni yangu ningeomba Katiba hii ikiwa ni bure basi iwe ni bure kwanzia dawati, kitabu, kalamu, majengo na kila kitu. Isipokuwa tu mazazi wakati ule mtoto wangu yuko primary level najishughulisha rasmi kwa kumpeleka secondary school. Sihusiki na mambo ya kalamu, dawati, daftari, hiyo yote serikali ifanye. Hiyo ndio elimu ya bure, lakini sio elimu ya bure na tunaitishwa kalamu na kitabu.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya afya. Katika hali ya afya maoni yangu mimi ningeonelea kwamba limeendelea ingawaje kiasi ya kwamba tunazidiwa tu bure. Ilikuwa cost-sharing, sasa imekuwa ni shida kwa sababu magonjwa yanatukabili. Utakuta ya kwamba mgonjwa wa kawaida hawezi kujipeleka hata kwa operation kwa sababu ya gharama ya pesa. Ikiwa huduma za afya ni muhimu kwa mwanadamu ziwe ni bure na kama kuna gharama serikali igharamie yule mtu ambaye anagonjeka hata kama ni Kenyatta National Hospital ama hata kama ni nchi za nje apelekwe akatibiwe arudi hapa akiwa mzima. Hayo ndio maoni yangu, asante sana.

**Emmanuel Karisa Kabombe:** Asante bwana Prof. Commissioner. Mimi yangu ni mawili tu. Ya kwanza inahusu jela. Umesema Commissioner yakwamba wale ambao wanaenda kule jela, Katiba hii mpya inataka kuwatunza kidogo wasiteseke. Lakini hapa naona Katiba imeacha kitu kidogo kwamba mateso ya kwanza hapa Kenya ni ile hali ya zile remand au cell au jela

zetu, hapo ndio tayari kunaanza hayo mateso. The rich yuko kule juu, yule ambaye amefanya uhalifu na yule ambaye bado kufanya uhalifu, wote wanateseka pale mahali pamoja wakilalia mavi na mkojo na mambo mengine. Kwa hivyo kuna hali ya kuangaliwa Katiba ya kwamba kwa kuwa suspect bado hajajulikana kama amekosea au la. Kuwe kuna hali ya kujua huyu atakuwa wapi na huyu atakuwa wapi lakini si kuchanganya watu hivi hivi na kule jela pia kuna hali ambayo kuna vifungo mbali mbali lakini hali za jela zetu za Kenya iko hali mbaya. Kwa hivyo Katiba iangalie kule jela kuko vipi, ndio kuna adhabu inatolewa hata pengine mtaondoa kifungu ile adhabu ya kunyongwa ndio tunasema kwamba kunyongwa kusiweko, lakini kule jela kuna watu wameshikwa na hatia mbali mbali pale kuangaliwe vile adhabu ya jela ziko namna gani. Na kule jela hali ya elimu ya wale watu kuwaelemisha wakitoka wawe raia wema izidishwe kama ni fundi wa kujenga azidi kujenga kama hajui kujenga afundishwe kujenga akitoka hapa aache wizi afanye kazi ya kujenga.

Ya pili ni ile uwezo wa rais ku-appoint wale watu (presidential appointments). Mimi ningeliomba ijapo ile presidential appointments zitaenda Bunge kwa kuidhinishwa, lakini yule rais mwenyewe awe na watu watamsaidia ku-appoint wale watu isiwe akili ya mtu mmoja kwa mfano hapa sasa kuna Tume ya Katiba. Kama Tume ya Katiba hiyo kwa kuwa imekaliwa na watu wenye elimu wenye fikra nzuri hata kule bunge inakuwa ni rahisi kupitishwa, lakini kama ni rais pekee yake ndio ana-appoint jaji, waziri, na wengine, kuwe na watu wachache watakaomsaidia rais ku-appoint wale watu kabla ya kuenda kule bunge kuidhinishwa. Asante Commissioner.

**Kahindi Katana:** Kwa jina ni Kahindi Katana. Jambo la kwanza bwana Commissioner nikependa kuwapongeza sana kwa kazi yenu ambayo mmeweza kuifanya baada ya kututembelea sisi kuchukua maoni yetu na kuiyaweka pamoja na kuyaleta tena kwetu ili tuweza kuangalia ni wapi tunaweza kurekebisha. Kuhusu mambo ya watoto, hawa watoto wasio na tabia njema imesemekana kuwa wanaweza kuchukuliwa hatua fulani imetajua kuwa wawekwe ndani kwa muda fulani lakini haikutajua ni muda gani. Pengine kwa sheria kama hii ikiwekwa kwa muda fulani anaweza kuchukua muda mrefu ingawaje umesema ni mfupi haikutajwa specifically kwamba ni muda fulani. Kwa hivyo naomba katika sehemu ile ya watoto kurekebishwe itajue kwa mfano kama atawekwa ndani mtoto yule kwa masaa kama ni mawili au kwa masaa kama ishirini na nne. Nafikiri hapo ingekuwa ni sawa sana.

Jambo la pili ni kuhusu powers za Parliament, hawa wabunge wamepewa uwezo wa ku-ammend Katiba. Ikiwa wamepewa uwezo wa ku-ammend Katiba sisi hapa tuna district government ambayo tutaipanga katika Katiba hii mpya. Sasa ikiwa watapewa powers za ku-ammend moja kwa moja katika zile nyumba mbili, mimi ni maoni yangu kwamba hizi district governments zipewe nafasi ya ammendments kama hizo katika hii Constitution waweze nao kuchangia ili waweze kutoa kwa mfano iwe wana uwezo katika ammendments ya constitution. District government ipewe uwezo wa kujadili na kukubaliana katika hiyo district. Kwa mfano wajadili na kupitisha kwa 75% wakisema tumekubali ndio hivyo imekubalika kabisa lakini sio tu Parliament pekee yake kule. Iwe district governments kama vile ulivyosema wa ammendments ya hii Constitution ili wao pia waweze kutoa mawazo yao na yafikiriwe ki-percentage – 75% ama 90%.

Jambo jingine ambacho ningetaka kuchangia hapa ni kwamba mumefanya kazi nzuri, mmesema kina mama wapewe nafasi nzuri kabisa na hii ni vizuri ndilo tulivyosema ndivyo tulikuwa tukililia tukisema kina mama wahusishwe. Je, kwa mfano katika wilaya ya Malindi, akina mama wasiweze kujitokeza tutawezaje kupata ile one-third ile ya akina mama. Kuna njia gani ambayo itatumiwa ili hawa akina mama waweze kupata nafasi hiyo ya one-third ikiwa wao wenyewe hawajajitoa kupigania kisiasa kama ni ubunge au kidiwani kama hawakujitokeza na katika wilaya itajazwa namna gani.

La mwisho kabisa kabisa ni kuhusu kufutwa kwa Prime Minister. Kama Prime Minister amefanya kosa fulani yeye anafanya yeye afutwe, sikuangalia sana lakini inaonekana ikifutwa yeye Prime Minister afutwe na waziri wake. Prime Minister akifanya kosa na pengine hawa mawaziri hawakufanya kosa ingawaje amewateua yeye. Kwa hivyo nafikiri hapo tuelezwe ama nyinyi mfanye uchunguzi na kurekebisha sehemu kama hiyo. Asanteni sana.

**John Diria:** Kwa jina naitwa John Diria, mimi ni mkaaji wa hapa katika mtaa wa Sabasaba. Nashukuru kwa Tume hii kupata kututembelea leo hapa na hivyo basi nina maswali kidogo ambao kwamba pengine yatakuwa ni maoni lakini vile ambavyo utayachukulia. Katika tawala ambazo kwa sasa zinaendelea tunaona ya kwamba kitu kinaweza tendeka na kikawa kimekwama lakini mtu yuajikadamiza hivyo hivyo. Tume hii nataka kutoka sasa itaweza kufikiria ya kwamba tatizo ya kifedha ndio tatizo kubwa kutoka kwa serikali mpaka kwa nyumba ya kila mtu. Kwa hivyo mara moja serikali inapokuwa na tatizo ya kifedha basi rais huyo lazima ajiuzulu kwa sababu atakuwa anatatiza wananchi. Hawezi kuwaendesha. Yale makadirio anayoyapata kutoka kwa wananchi hawawezi kuyapanga sawa sawa na mahitaji ya watoto wake. Kama mimi niwe nyumbani kwangu inahitajika mfuko miwili ya unga halafu niende na nusu mfuko unafikiri watoto wangu wataridhika, watalia sana na kama sitawapa jawabu basi watoto wale mara nyingine wanaweza kunipiga kabisa. Tume hiyo iangalie na iweke sheria ambayo kwamba itachunguza hali hiyo. Pia ninaiomba Tume hii ikaweze kukaa, si kwamba tuna tatizo la kifedha basi tatizo hilo linapatikana tu katika serikali yetu kwa sababu ati hakuna pesa. Pesa mara nyingine huwa ziko lakini kuna ukosefu wa Tume maalum ambazo zinachunguza ile miradi ambayo inatakikana iendelee kwa wakati fulani. Na hivyo basi utapata mafanikio yanakuwa ni hafifu, mjaribu kurekebisha sana sehemu hizo.

Sehemu ya pili ambayo nataka kupeana kwa Tume yetu ni kwamba katika kila wilaya ni lazima iwe na rasilimali asali, yaani zile ambazo zinapatikana kule. Zile ndizo ambazo zinaonyesha pato la wananchi. Kwa mfano hapa mkoa wa pwani tuko na mnazi kwa wingi, tuko na mwembe na miti mengine, ile ndio inachangiza kabisa hatua ambayo kwamba sisi tungeweza peana kodi fulani kwa serikali ili tuweze kujiendeleza. Maofisa ambao watakuwa na utalamu wa mimea kama hii waweze kuletwa na pia waweze kukadiria ni mimea aina gani ni nzuri ambayo kwamba itaweza kutuendeleza katika hali ya kujitoa umasikini wetu. Maanake ile raslimali na mimea yote ambayo kwamba imekuwa ikituendesha yote sasa haifanyi kazi, mwanadamu amekuwa hapa coast lakini tumekuwa tuna shida nyingi sana. Tume hiyo ikafikirie njia gani katika kila sehemu ya nchi ni mmea gani unaweza kushtawisha wananchi na wasisitize na iwaeke sheria ili hali hiyo iweze kuendelea. Pia wapeana katika masoko yao bei maalum ili ninapotoa kitu changu niwe najua nitaenda wapi. Kwa mfano mimi nina kuku wangu nawauza pale lakini sijui nani anahitaji kuku na sijui ni wapi nitapeleka kuku. Je wananifaidi wale kuku? Itabidi ni wale, nitazunguka labda wewe huna namba

ya kuonyesha unahitaji kuku. Asante.

**Speaker:** (inaudible)

**John Diria:** Tunahitaji kuwa na mapendekezo ya masoko maalum na bei ambazo zimepandishwa. Ninashukuru kwa nafasi hii mapendekezo yangu yalikuwa ni hayo.

**Joshua Charo Kazungu:** Prof. Idha karibu Gongoni, wageni wote mliofika karibuni. Mimi nina sehemu tatu. Nitazungumzia sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ambapo ni the Land Act na tayari Professor alituelezea kwamba kuna muda wa miaka miwili serikali itachunguza, ni ombi langu kubwa maana ardhi ndio hai. Mimi ni ofisa niliyestaafu kutoka wizara ya kilimo, retired agriculture officer. Ardhi ni kitu cha muhimu, ni uhai wa binadamu, hilo swala la muda wa miaka miwili ni sawa, nakubaliana nalo lakini liwekwe mkazo maana bila ardhi hatuna uhai. Ni kitu cha maana kwamba niweze kumiliki ardhi ile nilionayo mimi nalizungumza nikiwa marafa na niligusia pale kwamba kama serikali imeona vyema kwa ardhi yake kwa sababu ardhi ni ya serikali imefanya demarcation ama land adjudication. Imenigawia ile ardhi imeona vyema niimiliki kusiwe na sababu ya mimi kuipata cheti cha kuimiliki ardhi ile mara moja kwa maendeleo ya ile ardhi maana bila kuwa na cheti mimi si kitu ama haitawezekana mimi niwe na maendeleo mazuri. Kwa hivyo hiyo swala la ardhi ni muhimu na ni muhimu zaidi.

La pili, the Banking Act, na hii kwa ufupi kwa maana nimezungumzia ardhi, leo ni nikienda Kenya Commercial Bank nikitoa cheti changu cha ardhi pale ninaonekana sihudumiwi vilivyo. Nafikiria hiyo Banking Act ingefanyiwa revision, maana kama mimi ni raia wa Kenya na ninacho cheti cha ardhi maana hicho ndicho wanachokitaka, kusiwe na vipengele vingi hata ionekana kwamba mimi si raia na mimi si mwizi nimetoa ni cheti changu hicho cheti kinafaa mimi nipewe mkopo niendelee na ardhi ambayo ninayo. Pale inaonekana nigarimikie tena mimi ambaye nataka kujiendeleza ili kuwe na maendeleo tuwe hatuna umasikini kenya. Kitu cha kwanza ni kuondoa njaa ndipo tutaondoa umasikini. Kwa hivyo the Banking Act ifanyiwe marekebisho kwamba nikitoa cheti changu cha kumiliki ardhi niweze kupewe mkopo unconditionally.

Tatu, the Pensions Act. Hapa nilizungumza wakati mwengine kuhusu wanaostaafu na watakaokuwa wanatarajiwa kustaafu. Ikiwa nimepata notice ya kustaafu mimi kwa muda wa siku tisini nitayarishiwe malipo yangu, siku ile ya kutoka nje cheki yangu iwe tayari sio kwenda Nairobi. Nikisema hivyo nilikuwa mwezi moja na nusu Nairobi nikitafuta haki yangu, maana niliwacha utumishi kwa sababu ya shida ya asthma, there is no prescription ya asthmatic people one earth, there isn't but I am lucky. I am fine I met with a company known as Switzgerd and I am normal now. Sasa mtu anapopata notice ya kustaafu iwapo ni ya mwaka au ni ya siku tisaini ikimalizika tu leo tarehe kumi na nne, kesho tarehe niko nje kumi na tano niwe nimefungiwa kesho niwe nje, hiyo ni muhimu.

La mwisho kabisa ni kwamba nimeelewa kwamba district kutakuwa na serikali. Kuwe na ofisi ya pension ili mambo yangu imalizikie hapa hapa, si lazima Nairobi maana kule nimeteseka mimi. Kuhepahepa magari napitia huku karibu kumalizwa mzee

mimi, kwa nini nisimaliziwe mambo yangu hapa na nikaachana na hapa. Hayo ni ya muhimu sana na ningeomba Commission hii Professor ukiwa Commissioner wetu wa kutoka kwetu hapa itiliwe maanani kwamba kuweko na ofisi ya pension hapa hapa tu wilayani, mambo yangu yamalizikie hapa hapa tu. Siku ile ya tisaini nichukue pale pale Malindi niende nyumbani huko nikapumzike. Asante sana.

**Sheikh Abdalla Sheikh:** Nashukuru ambao wahusika katika jambo hili maanake labda mpaka kufa kwetu hatutalipata tena, kwa hivyo mwenye dukuduku lake afadhali alitoe hapa. La kwanza nimeshukuru lakini katika kueleza kwetu na mimi sina ile karatasi, kama nimekosea haiko pale mtanijulisha. Mambo ya mipaka katika eneo letu la Kenya, katika mkutano tulipokuweko tumesisitizwa zaidi katika mipaka kama ya Kenya, Uganda, Tanzania, lakini hatukutiliwa mkazo mpaka wa bahari ambayo ni maili ngapi na ni maili mia mbili ya ile international au ni vipi katika bahari yetu. La pili, tukija katika investors, madamu tumeona kuna mambo ya globalisation ambayo yamempa yule tajiri aliyetoka nje aje alete uchumi wake hapa, lakini katika ule uchumi wake utadhorofisha wachumi wadogo wadogo. Kwa mfano bwana mmoja ametoa hapa habari ya kuku. Ninaweza kufuga kuku mia moja mia mbili lakini akaja mtu ambaye ni investor akafuga kuku milioni moja hapa, hii biashara yangu itakwenda wapi ya kuku mia mbili?

La tatu kuna habari ya consumers rights ambao wateja haki zao namna gani, hatukuona kuwa imeelezwa hii wateja. Leo tunaona kila siku watu wa power and lighting, watu wa simu wanamaidara nyingine nyingine watu wakupandisha vyakula vinapanda hasa hawashauriwi wale wateja haki zao, wanaweza kumiliki kununua kuhudumia au kulipa huduma walizopewa zile. Kwa hivyo tunataka iangaliwe zaidi juu ya mambo ya consumers rights. Nyingine ni wafanyi biashara walioandikwa kazi wanaweza kuenda on strike. Je, imefikiriwa wakati wale wamekwenda on strike watapata wapi malipo yao kwa hivyo wasione kuwa ile strike yao si ya halali wakalazimishwa kwa kuwa hawana malipo ya kulipwa kuwa wavunje ile strike na hali wanayo haki zao. Mfano ni ya walimu waliofutwa.

Jambo lingine ambalo mtanisamehea nitasema kwa ufupi ni mengi kidogo. Ni habari ya kuhesabia kura katika vituo. Hili si jambo ambalo ni rahisi lakini je mtatoa mambo ya computers ambazo results zikihesabiwa kama kituo cha hapa na kutolewa nani mshindi labda itakuwa Malindi, si itachukua siku kadha kusafiri hapa mpaka kule ama vipi? Je mtaweza ku-establish computers ambazo zitaweza kuwakilisha mifano kama hii. Ingine ni juu ya election. Hapa tumetajiwa kuwa atakayeshida hata kama ni kwa kura mbili atapewa ushindi. Je, hilo limehakikisha kuwa yule mwenye majority wins amepata maanake inawezakuwa watu wamesimama watu wanne watano, lakini kila mmoja hakupita zaidi ya 50%. Je hiyo itakuwa ameshinda kwa wingi au itakuwa amekosa kwa shauri kitangamanisho waliopiga kura watu wengine ni nyingi zaidi kuliko zake. Tunataka liangaliwe kwa hakika hiyo ya majority tuambiwe anayepita.

Nitatoa maelezo zaidi katika habari ya huyu Prime Minister. Yeye atakuwa ni anasimamia mabunge yote mawili au ni hiyo moja tu ya national council? La mwisho ni qualifications za watu watakaochaguliwa katika baraza la wilaya. Asante sana.

**Reuben Kenga:** Asante sana kwa kupata nafasi hii kueleza maoni yangu kuhusu mswada wa katiba yetu. Ningetaka kueleza juu ya haki ya uhuru wa mtu, hapa imeandikwa security of the person. Hapa imeeleza kwamba mtu ana haki ya uhuru na pia ana haki ya ulinzi, alindwe popote anapoishi apate ulinzi kamili. Pia ikaendelea kueleza ya kwamba anapokusa anapowekwa rumande si haki anyanyaswe, pengine kutukanwa, kupigwa na kadhalika. Haya ni maoni mazuri, lakini iwapo mtu ama mshukiwa atatiwa nguvuni na kutiwa katika rumande na anyanyaswe, apigwe, atukanwe na alazimishwe kusema mambo ambayo si sawa. Mtu kama huyu atafanya aje, lazima apewe nafasi ya kujitetea ili kunyanyasa kwake, kule kununuliwa kwake kujulikane ili ajitambue kutokana na hali ile ya kunyanyaswa. Hapa katika Katiba mtu huyu ambaye ananyanyaswa katika rumande hakupewa nafasi, tumeamibwa kwamba tu hana haki ya kunyanyaswa na asiwekwe rumande kwa zaidi ya masaa arobaini na nane. Lakini iwapo amewekwa rumande kwa zaidi ya masaa arobaini na nane, Katiba haikumpa fursa huyu mtu kujitetea kujitambua kutokana na shida hii. Kwa hivyo apewe nafasi hapa iwapo atazuiliwa kwa zaidi ya masaa ya arobaini na nane, lazima apewe nafasi atafanya aje na iwapo atanyanyaswa kupigwa, kuteswa, kudhulumiwa pale rumande lazima huyu mshukiwa apewe nafasi ya kujitetea, atafanyaje? Kwa hivyo Katiba pale impatie nafasi si kumwambia tu asizuiliwe kwa zaidi ya masaa arobaini na nane.

Sehemu nyingine ni kwamba umilikaji wa ardhi, tumeambiwa ya kwamba mtu ambaye si raia wa Kenya, hana ruhusu kupewa kibali cha kumiliki ardhi ni sawa. Lakini akaambiwa ya kwamba apewe ruhusa ya kukodisha ardhi kwa miaka tisaini na tisa, hii ni kama kumpatia ardhi maisha yake yote, ni mingi sana ipunguzwe. Ni nani ambaye anaishi miaka tisaini tisa? Hakuna, ni kama kumpatia ardhi aimiliki kwa maisha yake yote na ikiwa mimi ninasumbuka kwa sababu huyu mtu ambaye si raia wa Kenya, pengine amepewa hii ardhi na ameistawisha pengine kwa miaka kumi na tano au ishirini hivi, nami najiona katika hali yangu ya kiuchumi ni nzuri sana, ninaweza hata kuistawisha zaidi ya vile alivyostawisha yule mgeni. Kwa nini aendelee kuikalia ile ardhi asistawisha. Mimi ningependekeza miaka thelathini, ikiwa ni nyingi pengine mtanisaidia katika swala hili. Kwa miaka thelathini pengine nitajifundisha kutokana kwake na nitajaribu kuistawisha ile ardhi. Maoni yangu ni kwamba huu muda ni mrefu sana upunguzwe.

Lingine umesema Professor ya kwamba baada ya kukamilisha huu draft, huu mswada wa Katiba yetu, serikali itapewa miaka miwili kusuluhisha tatizo ya ardhi ili hii tatizo yetu ya ma-squatter. Tatizo hili la kumiliki ardhi hapa kwetu pwani tatizo hili liondolewe kabisa kwa mara moja kabisa lisitutatize tena. Lakini ningeongeza kwamba hii Commission ya kuchunguza malalamisha ya ardhi inapoanza kazi, ishirikiane na haya mabaraza ya wilaya ambayo umesema ya kwamba yatachaguliwa ili kuonyesha maendeleo ya kila wilaya badala ya jimbo nzima ukasema tumechagua wilaya. Hii Commission inapozunguka ishirikiane kwa hali yote kabisa na vile vya baraza la wilaya katika uchunguzi wao ili sisi tuendelee kwa lolote lile. Mimi naona wakishirikiana vyema na hili baraza la wilaya matatizo yatamalizika, lakini hili baraza la wilaya likiwekwa kando, tukiacha kazi yote kwa ile commission ambayo itaanza kuchunguza malalamishi ya ardhi, mimi ninaona kazi yao haitakuwa nzuri, kutakuwa na malalamishi tena. Washirikiane kwa kamilifu kabisa na wenyeji wa wilaya ile kuchunguza malalamishi ya ardhi. Asante sana.

**Com. Idha Salim:** Asanteni sana kuna ishara nzuri kwamba tumeshaanza kuisoma hii Katiba na kujaribu kuifahamu na Mungu

akipenda mtaendelea kufanya hivyo hivyo na mtupe maoni kama hayo hayo mtatuandikia, mtatuletea kufuatana na mikono ya District Coordinator wetu na members of the committee watupelekee Nairobi. Maana kama nilivyosema hapo awali hii si Katiba ya mwisho, hii ni mswada wa Katiba, kwa hivyo itaendelea kuchimbuliwa na kutengezwa mpaka tufike siku hiyo ya mwisho yakupitishwa bungeni. Kwa hivyo tungali tayari kusikiza maoni yenu. Kwa haraka kabisa nitajiribu kuwajibu hawa jamaa waliotuuliza maswala hapa na pale.

Tutaanza na Bwana Samuel arap serem. Nafikiri Bwana Samuel alitaka kujua hawa Ministers watachaguliwa vipi. Kama nilivyosema hawa watachaguliwa kutoka nje, vipi watachaguliwa itategemea yule Prime Minister atakayewapendekeza au recommend – mimi nataka Minister wangu wa hivi awe ni fulani, qualifications zake ni hivi na hivi. Kwa hivyo kutakuwa na majadiliano juu ya kila mmoja wao katika Bunge. Bunge lazima ipitishe kila mmoja wao na haitampitisha mtu kwa kuwa fulani anampenda. Wabunge watakuwa mia tatu, kwa hivyo bila shaka kila aina ya swala litafanywa na kisha pia wajua bunge itakuwa na kamati zake, kamati ambao itaanza ile kazi ya uchunguzi katika hawa Ministers. Kwa hivyo kutakuwa kila njia ya kuhakikisha kwamba yule ambaye mwishowe atakuwa Minister, ni mtu ambaye bila shaka alipita pingamizi nyingi sana akaziruka hata akapita kuwa Minister. Wataulizwa maswala, watafanyiwa uchunguzi na kadhalika kabla hawajapitishwa. Hakuna njia yoyote ambayo mtu mmoja binafsi au watu wawili watatu watampitisha mtu awe ni waziri au naibu wa waziri au makamu wa rais.

Swala la pili yahusu capital ama raslimali. Kutakuwa na council maalum inaitwa council ya uchumi na mambo ya kijamii. Kwa hivyo jambo kama hili litatizamiwa kwa uzuri sana na mambo ya capital na investment yatachambuliwa vizuri sana. Bila ya investment, bila ya raslimali itakuwa ni taabu sana kuendesha nchi yeyote namna itakavyokuwa kwa ile constitution yake. Kwa hivyo mambo haya yamewekwa utaratibu wake sawa sawa na ukisoma hii Constitution section inayohusika na mambo ya uchumi, utaona section maalum inaitwa Economic and Social Commission. Kwa hivyo jambo hili limezungumzwa hapo.

---

Labour – pia sikufahamu habari ya minister. Ulisema nini habari ya labour Bwana Swaleh?

---

**Speaker:** (inaudible)

---

**Com. Idha Salim:** Mazingara ya kazi ni jambo muhimu sana hili, nimezungumza habari ya wafanyi kazi. Nilisema kwamba mfanyi kazi ni lazima apate mshahara ambao ni mshahara mwadilifu ambayo ni just and fair. Pia mazingara ni muhimu sana kuwa ni mazuri na kama nilivyosema pia hii Katiba ndio Katiba baba. Chini ya Katiba baba kutakuwa na sheria nyingi sana kwa hivyo kutakuwa na sheria inayohusika na kazi na mazingara ya kazi na mambo kama hayo itafanywa na Parliament. Ukitizama katika huu mswada huu wa Katiba tumesema kwamba jambo hili lichunguzwe au lifuatwe kufuatana na sheria ambayo itapitishwa na bunge. So we are looking forward au tunataraji sheria zingine ambazo zitasaidia sheria hizi tulizozitaja. Ikiwa tutataja kila kitu katika Katiba, basi Katiba hii ninakuhakikishia itakuwa ni kubwa sana. Kwa hivyo tunafikiria hii sheria

ndio sheria baba na sherehe zingine zinazohusika kwa mfano hapa na mambo ya kazi na mazingara ya kazi zitatajika. Nilitaja hapo awali pia taabu za wafanyi kazi, wanaofanya kazi katika mitambo ambapo mazingara ni mabaya na ni hatari katika maisha yao na afya yao. Kwa hivyo haya ni mambo bila shaka lazima yazingatiwe na kanuni kama hizo ziwekwe kuisaidia hii Katiba kutimiza muongozo wake.

---

Joseph Karai umesema kwamba child employment au kazi za wafanyi kazi ni kwa ajili ya watoto kuambiwa wafanye kazi wauze hili au lile barabarani na kadhalika ni kwa sababu ya umasikini. Maoni hayo nakubaliana nayo, lakini pia tufikirie kwamba hali lazima itengezwe kama nilivyosema wafanyi kazi wapate hiyo mishahara mizuri ili kwamba mtoto badala ya kufanya kazi kusaidia jamaa yake aweze kuenda shuleni badala yake na kusoma kuwasaidia kwa njia ya kusoma apate kazi na awasaidie wazazi wake. Pia ukifikiria district government niliyozungumzia ni kwamba mambo kama haya yatafikiriwa sana na district government. District government itahakikisha kwamba kutakuwa na elimu, itahakikisha kwamba kutakuwa na matibabu au matumishi ya matibabu katika wilaya hilo. Kwa hivyo matatizo mengi ya mtoto na mfanyi kazi ni kati ya matatizo ambayo itasaidika kufuatana na sreikali ya wilaya kufanya kazi zake kama ilivyotakikana.

---

Raslimali au mali asili ya nchi, tumedokezea kwamba district government au serikali ya district itakuwa ikipata msaada kutoka serikali ya kati khudi la pesa, juu ya zile pesa zitakazopatikana kutokana na njia zingine ambazo zitapatikana kutokana na njia nyingine ambazo zitatumiwa na serikali ya wilaya kupata pesa. Kwa mfano kodi ambazo zitakusanywa katika wilaya zitabakia pale pale na juu ya hivyo pia serikali ya kati itakuwa ikisaidia kupeleka ustawi katika kila wilaya kutokana na pesa ambazo zitatoka kule Nairobi. Lakini hata hivyo mtaona kwamba tumesema kwingine kwamba sehemu kubwa ya mapato ya mali ya asili katika eneo fulani itatumiwa pale pale. Kwa mfano hapa mikoko ama mangrove, sehemu kubwa ya mapato au faida ya mikoko itatumiwa hapa hapa katika eneo la Malindi. Pia kule bandari ya Mombasa, kutoka kwa utalii, sehemu kubwa ya mapato haya – kutakuwa na record ya mapato, bila shaka kutakuwa na evidence sisi tunapata kitu gani katika utalii. Kwa hivyo tunasema ama tunapendekeza sehemu kubwa ya mapata hayo kutoka mali ya asili katika eneo lolote itatumika pale pale. Haya yote tumeyataja katika mswada huu.

---

Stephen kombe umesema kwamba kwa nini Rais hachaguliwi na watu, lakini hatukusema kuwa Rais hachaguliwi na watu. Rais atachaguliwa na watu kutakuwa na uchaguzi wa rais, kutakuwa na uchaguzi wa rais kwa kura na wananchi na uchaguzi wake utakuwa mbali na uchaguzi wa Mbunge – two different elections. Kwa hivyo Rais atachaguliwa na wananchi.

---

Maji na umuhimu wa maji, kwamba maji iwekwe katika mstari wa kwanza pia tumesema. Katika haki za kibinadamu ile kanuni ya haki za kimsingi haki ya maji imetajwa hapo. Kisha tukumbuke kwamba district government pia ina kazi ya kuhakikisha kwamba watu wa Malindi wanapata maji ya kutosha. Itakuwa ni jukumu lao kuhakikisha kuwa watu wa Malindi tunanjia ya kupata maji hapa, maji ya Malindi inafika mpaka Mombasa. Kwa hivyo ni kazi ya serikali ya wilaya kuhakikisha kwamba watu wake wanapata maji ya kutosha. Pia mambo ya wafanya kazi katika maeneo ya chumvi tumetaja kwamba

---

mishara lazima yawe ni bora zaidi na pia wale matajiri wanaoendesha factory hizo za chumvi au yeyote, wahakikishe kwamba wananchi wanatunzwa wanapewa vifaa ambavyo vitawalinda dhidi ya matatizo yeyote ya kazi yao. Utaona kwamba kule nchi za Ulaya na Amerika na kadhalika kuna njia ya kuwalinda wafanyi kazi, wanafunukiwa kwa macho ama mikono ama pua kuhakikisha kwamba hawadhuriki na kazi yao. Hapa pia ni kazi ya serikali ya wilaya ili iweze kuweka zile by-laws ambazo zitawalazimisha hao matajiri kuwalinda wafanyi kazi wao na kuwasaidia kufanya kazi katika hali ilio nzuri.

---

MPs tunasema kwamba lazima MP a-report. Tumepata malalamiko kwamba MP baada ya kupigiwa kura anapotea, harudi tena kule. Kwa hivyo tunasema kwamba huyo lazima afanye kazi yake na wajibu wake, asipofanya pia tumeeleza jambo ambalo sikulitaja mimi lakini liko hapa kwamba tumesema kwamba ikiwa wale wanaompigia kura katika ile constituency yake hawakutosheka, wana njia ya kumshtaki kupeleka barua ya mashtaki kwa clerk of the National Assembly. Clerk of the National Assembly atafanya committee yake kufanya uchunguzi juu ya malalamiko yeyote ya wale raia ambao wako katika hiyo constituency. Na kuna njia kwamba baada ya uchunguzi utadhibitisha kwamba huyu jamaa hakufanya kazi yeyote anaweza kuondolewa. Kwa hivyo tumeeleza njia ya kumuondoa Mbunge katika eneo lake. Pia tumesema kwamba Mbunge asibakie zaidi ya miaka kumi, achaguliwe miaka mitano ya kwanza na ikiwa watu watafurahi si watamchagua tena mara ya pili? Watamchagua mara ya pili, lakini baada ya hapo mkifurahi msipofurahi ataondoka lazima mchague mwengine – two year term. Rais ni vile vile miaka kumi. Rais atafanya kazi miaka mitano kwanza, kisha akitaka kusimama tena atasimama atafanya kazi miaka mitano mengine lakini baada ya hapo ataambiwa basi asante sana apewe retirement benefits zake na aingie Rais mwengine. Kwa hivyo hakuna mtu atakeyedumu katika utumishi wa wananchi, miaka mikumi ndio maximum – kiwango cha juu kabisa.

---

Bwana Emmanuel masha umeuliza habari ya natural resources, nafikiri nishataja mambo ya mali ya asili. Mangrove industry, nafikiri nimeeleza kwamba mangrove industry ni industry ambayo ni muhimu kwa wananchi, natural resources pia ni muhimu na nishaeleza kwamba mali ya asili ni lazima itumike kwa maslahi ya wananchi. Ile sehemu ambayo itakwenda kule central government au Nairobi pia igawanywe kwa njia ya uadilifu, nilisema hapo awali. Kwa njia ya uadilifu maanake ni kwamba kila eneo ya Kenya ifaidike kwenye mali ya asili ya umma, kodi zitakazopatikana kule treasury Nairobi ili zitumiwe kwa faida ya kila eneo ya Kenya. Lakini juu ya hivyo tumesema kwamba serikali ya wilaya pia itakuwa ikipokea kodi tuseme kutoka masoko, kodi hiyo pia itatumiwa katika masilahi ya wananchi. Basic education, elimu ya msingi ugependa kweli iwe ni ya bure. Tumesisitiza kwamba itakuwa ni haki yake mwananchi katika ile bill of rights au kanuni ya haki kwamba elimu ya msingi itakuwa ni ya bure. Hapo ikiwa hamkupata elimu ya bure mnaweza kushtaki, mtaseme kwamba hii ni haki yetu chini ya Katiba sio chini ya sheria yeyote or Education Act, iko chini ya Katiba juu, kanuni baba au sheria baba. Kwa hivyo mtu anaweza kwenda kotini akaseme kwamba mtoto wangu nimempeleka shuleni akataka kutozwa fees na mimi ninakataa. Nataka koti iweze kusema mtoto wangu aweze kuenda na hana haja ya kulipa chochote na koti itapitisha hii. Ni muhimu sana mtu kunyimwa haki zake.

---

Kwa hivyo kuna haja ya elimu ya raia katika mambo haya ya Katiba. Saa zile tukizunguka hapa na pale kupokea maoni yenu tuliwaambiwa kuwa maoni yenu ndio yatakayotiwa katika Katiba na kisha itakuwa ni nyinyi kuilinda ile Katiba na mna haki ya kuilinda ikisha kupitishwa katika Bunge, na kuilinda ni vipi? Kuitetea, mkiona inavunjwa muende kotini na kama nilivyowaambia hakuna haja ya kumlipa Bwana Sharma au lawyer fulani pesa, mnaenda kwa public defendor, mtetezi wa umma kushtaki jambo kama hiyo. Tumeweka Tume hapa na pale. Kuna Tume moja muhimu zaidi inaitwa Human Rights and Justice Commission, Tume maalum imewekwa kutizamia raia haki zake na justice – uadilifu, uadilifu ni kitu muhimu sana. Kuwa mambo yanaendeka kiuadilifu, hakuna anayelemewa, hakuna anayedhulumiwa. Kwa hivyo kwa hii Tume mtu anaweza kuenda kuishtakia ikiwa hakupata haki yake yeyote. Kwa hivyo ni mtu kujua kwamba iko haki hiyo, kujua kwamba iko Tume hiyo, ofisi yake iko wapi na bila shaka itakuwa ni Tume ya wenye ofisi kila mahali nchini, sio Nairobi pekee yake. Kwa hivyo ni nyinyi kujua haki zenu na kujua zile njia ambazo mtazitumia kupata haki hizo.

---

Matibabu, kama nilivyowaeleza, serikali ya wilaya pia ina wajibu wa kutoa huduma ya matibabu. Kwa hivyo ikishapata pesa hapo hapo, Malindi inapata pesa kwa mangrove, kwa utalii, serikali inaipa pesa, ni wajibu wa ile serikali ya wilaya kutimiza kazi zake, kuhakikisha kwamba kazi zake zinafanywa na mwananchi anapata zile huduma ambazo pesa zimewekewa. Ni mwananchi kutetea haki zake.

---

Emmanuel Karisa unasema kwamba hali ya jela ni mbaya sana, kwamba mtu anaketishwa, anadhulimiwa. Tumeeleza kwa urefu hapa haki ya mshtakiwa na haki ya yule anayeshukiwa kwamba amefanya kitu kibaya au amevunja sheria. Tumetaja kwamba asipigwe, asifungwe zaidi ya masaa arobaini na nane, lazima atolewe baada ya hapo. Ikiwa hajatolewa, jamii yake inaweza kuenda kushtaki kwamba huyu tangu siku fulani yuko pale hajatolewa. Kwa hivyo police officer yeyote concernced anaweza kupelekwa kotini kuulizwa kwa nini wewe unamweka zaidi ya masaa arobaini na nane. Tumesema pia apewe chakula, apewe matibabu ikiwa amepata ugonjwa kule jela, amewekwa tu kungojea hukumu yake, ana haki ya kudai matibabu apewe medical treatment. Yote haya tumeeleza kinaganaga katika hii Katiba. Nafikiri wengi hawajapata ile nafasi kusoma yaliyomo, lakini kama nilivyosema mtachakua fursa hii sasa mna nakala au copies, mtasoma vizuri. Tuna pia kiingereza na Kiswahili, juzi Taifa Leo ilitoa nakala ya Katiba kwa lugha ya Kiswahili. Leo tumetoa za Kiingereza, ziko za Kiswahili na huenda tukazipata zingine tukaziweka kwenye documentation centre, kituo chetu ambacho kinasimamiwa na Kinga Jeffa hapa mkazisoma hii Katiba kwa lugha ya Kiswahili pia. Samahani ninaenda mbio maana wakati unazidi kupungua.

---

Kahindi Katana umezungumza juu ya watoto na haki zao. Kweli tumetaja haki za watoto hapo, sikumbuki swala lako kuhusu watoto. What was the question kuhusu watoto?

---

**Kahindi Katana:** (inaudible)

---

**Com. Idha Salim:** Kwa hakika ule muda hatukutaja, ikiwa tuseme watoto ni watukutu wamefanya jambo mbaya or

something, lakini tumesema kwamba wawekwe kwa muda ambao ni mfupi kabisa ambao ni lazima awekwe katika muda huo. Lakini tumerekodi your note or your observation na huenda jambo hili huenda likazungumzwa katika hiyo conference kubwa kule Nairobi, lakini ni jambo muhimu umelitaja. District government ungependelea kwamba serikali ya wilaya pia ijadiliana juu ya Katiba kabla haijabadilishwa. Hiyo ni pendekezo ni muhimu hilo lakini tujue kwamba kuna mambo fulani ambayo hayawezi kubadilishwa kabisa ila kwa njia ya referendum, wananchi wote lazima washiriki. Ni mambo matano au sita ambayo hayawezi kubadilishwa kabisa, kwa mfano Bill of Rights. Haki za mwananchi zote nilizowatajia na ambazo ni nyingi, tumesema kwamba hakuna hata Parliament yenyewe haiwezi kubadilisha sheria hiyo. Ikitaka kuibadilisha kwa mfano, haki za watoto au haki za walemavu, Bunge haiwezi lazima wananchi waulizwe. Idadi kubwa zaidi ya wananchi, which is the whole population, lazima iulizwe je, tubadilishe hapa tumeseme hivi au vile, lazima wananchi waulizwe na wao ndio watakaotuambia. Na kisha ukasema kwamba ikiwa haiwezekani thuluthi ya wagombea wachaguzi wanawake tufanye nini? Hapo itakuwa si makosa yetu, tumejaribu hawakutokea, itabidi kuwachukuwa wale ambao wako. Na hapo ndio ninaambia akina mama mpaka sasa kama muonavyo akina mama ndio idadi ndogo zaidi hapa waliofika kusikiza mambo haya ya Katiba. Idadi kubwa ni akina baba na saa zote kila tukizunguka hapa na pale, tuliimiza kina mama waulize maswali na mpaka sasa sijaona mama mmoja kuja mbele kutuuliza swala lolote.

---

---

---

Pia tumepeleleza kwamba na tumewaambia kina mama hapa na pale kwamba mara nyingi kina mama wenyewe huenda wakampigia mwanamume badala ya mwanamke. Kwa hivyo ni juu yao kujisaidia kuwekwa katika vyama vyao vile kuelezana juu ya umuhimu yao pia kuwa katika safu ya mbele katika kuwakilisha wananchi wa kila aina, akina mama wawakilishe wanaume pia na kadhalika. Kwa hivyo it is a matter for them to take action lakini tumedokezea tu hapa kwamba vyama vya kisiasa viweke one third reserved for women candidates. Pia kwamba katika wale ambao watawekwa mbele kisha ile list mmoja mwanaume na wa pili ni mwanamke na tuombe ya kwamba wakati huo mwanamke mmoja ambaye yuko katika hiyo list asimame kina mama watampa yeye kura zao. Lakini wajua kina mama pia ni kama akina baba, huenda yule mama labda hana uwezo au wafikiri kuwa hana uwezo wa kuwakilisha vizuri na ukempendelea afadhali mwanamume ambaye ana uwezo kuliko mama ambaye hana uwezo. Kwa hivyo we have to leave it to them, tuwachie wao lakini tunasema kwamba wajaribu kadri iwezavyo kujitumikia wao ili wananchi wananchi watumikie wao.

Prime Minister dismissal – nafikiri hapa ulisema kwamba ikiwa--------------

(Interjection)

**Com. Idha Salim:** Maanake ile ni serikali, ni kama jamii. Serikali ya Prime Minister ni kama jamii yake, family yake, na ukimuondoa yeye afadhali uondoe family yake nzima. Maana kuna ile divided loyalty, loyalty yao ni kwa kiongozi wao yule Prime Minister. Kwa hivyo kila nchi inafanya hivyo, kwamba Prime Minister akiondoka, dissolve ile serikali, inaundwa serikali

mpya kabisa na Prime Minister. Pia yule Prime Minister angependa akuwe na team yake yeye mwenyewe ambayo yeye anapendelea ili kwamba ile kazi ifanyike vizuri zaidi. Kwa hivyo lazima apate wale ambayo yeye ana confidence nao. Lakini naye pia na team yake mpya huyo Prime Minister mpya lazima apate ile confidence au vote of confidence ya Bunge. So a clean house, clean break from the previous government.

Bwana Biria – public expenditure, planning development. Kwa hakika nafikiri sikufahamu sana, ila nikwambie tu kwamba sasa kutakuwa na mambo wazi wazi. Matamuzi ya serikali yatawekwa wazi wazi ili kwamba tujue development plans or planning development itakuwa ni kazi ya serikali ya kati na pia kwa ustawi wa wilaya ni kazi ya planning katika district itakuwa pia ni kazi ya serikali ya wilaya, lakini kutakuwa na coordination. Kutakuwa na body maalum au chama maalum ambacho kitafanya coordination kushikamanisha kazi ya serikali ya kati na serikali ya wilaya kuhakikisha kwamba mambo kuhusu maendeleo inafanyika kwa njia inayofaa.

Joshua Charo Kazungu, maoni yako ni muhimu sana – Land Act. Unasema kwamba miaka miwili kuwa ni ndefu sana, ungependelea mambo iende haraka. Sisi tumeweka kiwango cha miaka miwili lakini huenda maendeleo yakafanywa within those two years, tukaona mabadiliko within one year, lakini kiwango kabisa cha mwisho ni miaka miwili. Lazima yale mambo tuliozungumzia hapo awali nikawaeleza jinsi ambavyo kwa mfano kusuluhisha kutatua mushkil au tatizo la ma-squatters, ikiwezekana katika mwaka moja. Pia tumesema kwamba rais atakuwa na kazi ya kutoa ripoti kila mwaka kwenye Parliament, ni maendeleo gani yaliyofanyika katika mwaka huu kuhusu jambo hili, kuhusu jambo lile na kadhalika na bila shaka jambo hili la ardhi ambalo ninakubaliana na wewe kamili (100%) ni muhimu sana na tumesema hivyo katika tangulizi cha ile section (sura) ya land utaona kwamba tumesema au tumetaja ule umuhimu ya ardhi na mashamba kwa wananchi. Kwa hivyo ni jambo ambalo tukiweka misingi mizuri na zile tume ambazo zinahusika na uadilifu na kadhalika mambo yatabadilika haraka.

Banking Act: Hii Katiba kwa hakika ni kama masikizano au contract baina ya wananchi na serikali basically, lakini the bank ni mtu wa tatu huyu na huwezi kumlazimisha yule ni lazima ufanye hivi. Ni jambo la kuelezana, jambo la kufahamiana na pia tuhakikishe kwamba mazingara yaliyoko ni mazuri ili bank iwe na confidence. Tumeambiwa kwa mfano land title deeds na zikirongo, kwa vile bank zingine zinaogomba kwamba nitachukua hii land title deed kisha nitaambiwa hii ni double allocation na kesho pesa zangu bank yangu itaruka. Kwa hivyo kuna haja ya kusuluhisha na kustawisha mambo mengi sana katika mambo hii ya ardhi na mambo ya mikopo, lakini kuna section hapa inahusika na investment na kadhalika na tunatumia section hiyo kuhakikisha kwamba ile mazingara yetu ya kiuchumi, mazingara ya investors, kwa wale ambao wameleta pesa zao kuziweka hapa na bank ni investors. Kwamba mazingara ambao tunayowawekea waje wao na wale ambao watajenga viwanda na kadhalika, mazingara hayo ni mazuri. Bila shaka ni jambo ambalo halitamalizika leo ama kesho lakini tutaendelea kushtawisha kama nilivyosema kwamba kuna kanuni nyingine ambazo zinafanywa. Banking Act kama usemavyo, it is liable for reforms, for revision, inaweza kubadilishwa ili kwamba mambo yasailike zaidi kwa wananchi na mambo ikibadilika yakiwa mazuri bila shaka banking laws zitakuwa rahisi zaidi kwa mwananchi kuzitumia na kufaidika nazo.

Pensions Act pia inahaja bila shaka kubadilika. Tumepata mabadiliko kwa wananchi kama ninafikiri pia nilitaja hivi leo asubuhi nikianza kwamba kuna wazee wetu ambao walikuwa civil servants, hata mimi na bwana Kazungu tulio-retire na retire benefits zetu zimebakia vile vile, twenty years later mtu anapata hela hizo hizo hazikubadilika. Kwa hivyo mapendekezo wananchi ni kwamba ile pension ifanyiwe review kila mshahara ikifanyiwa review. Kwa hivyo kama nilivyosema pia tuna Tume maalum on Salaries and Remuneration Commission, hiyo ndio itaandika kiwango cha mishahara na bila shaka kazi yake pia itahusika na pensions. Pia tusisahau kwamba kuna Human Rights and Administration of Justice Commission. Hii kazi yake ni kuhakikisha mambo yanafanyika sawa sawa kuna uadilifu, kwa hivyo mtu anaweza kwenda na ana-petition kwenye Tume hii na kusema pension ya wazee walio-retire hazitoshi, maisha imekuwa makali zaidi kuna haja kuzi-review. Kwa hivyo tunaweza kutumia njia nyingi za kubadilisha mambo. Na pension services pia it is a matter of detail, ili kwamba ofisi ya pension ipatikane kwa njia ya urahisi kwa kila mwananchi asiwe na haja ya kwenda Nairobi kuchukua pesa zake na kujihatarisha kama vile alivyofanya Bwana Joshua hapa.

Bwana Sheikh Abdalla Sheikh, swala lako nafikiri la kwanza ni juu ya boundaries. Kwa hakika tumetaja habari ya boundaries kwa upande wa bahari, it is 200 miles extension. Price control na customers tumetaja hapa section maalum juu ya customers. Kwamba customers wapate manufaa, wapate value for money. Lile jambo ambalo nitalinunua cheap na ambalo litanivunjikia kesho, ninanunua leo na kesho chavunjika pesa zangu zikaenda bure. Kwa hivyo tumeweka section ambayo kinahusika na mambo ya customers na haki zao, lakini tukasema kwamba mambo haya haiko katika Constitution hivi sasa. Ni jambo ambalo tumesema tuipe serikali muda kuweka sheria kuhusikana na mambo ya customers rights.

Strikes rights: Kama nilivyosema nilisema anayo mtu lakini tusihukumu mambo yalivyo hivi sasa, tumependekeza mabadiliko hapa. Tuombe kwamba mabadiliko yakifanyika walimu na wengine waki-strike watakuwa strike yao ni ya haki na watakuwa kwamba washa-exhaust, washamaliza kabisa njia zote zile ambazo huenda zikawekwa ili kwamba baada ya kufuatwa kabisa ndio strike itatokea. Lakini ikiwa mechanisms au zile tools au zile ala kati ya wafanyi kazi na matajari yatawekwa uzuri, strikes au idadi ya strikes au kugoma zitapungua pia. Ikiwa hali hali nzuri zaidi au uhusiano bora zaidi kati ya matajiri na wafanyi kazi au kati ya serikali na wafanyi kazi vitawekwa vizuri zaidi. Na kama nilivyomweleza mwenzetu Bwana Charo, ile Salaries and Remuneration Commission pia itazungumzia wafanyi kazi wa serikali kama walimu na pia kuna Teachers Service Commission, tumehifadhi hiyo itaendelea. Kwa hivyo bila shaka salaries za walimu zitafikiriwa, review of salaries itafikiriwa na kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na hiyo Tume ambayo itakuwa permanent, hiyo commission ndio itasema kwamba Wabunge watapata mshahara gani, rais atapata mshahara gani, pension yake itakuwa vipi na kadhalika. Kwa hivyo kwa sasa tusi-judge mambo ya sasa, tu-judge mambo ambavyo yatatokea tukishaweka hii sheria kuwa ni sheria yetu.

**Speaker:** (inaudible)

**Com. Idha Salim:** Wajua bwana Sheikh hapa wewe unalinganisha au kuunganisha jambo ambalo liko sasa, walimu wa leo na jambo ambalo sisi tunafikiria kwamba litafanyika ikisha hii Constitution kupita. Ikishapita hii Constitution, mambo kama haki

zao na kila kitu zitaingia chini ya a new constitution na kama nilivyosema kuna tume kadha wa kadha ambazo haki ya mfanyi kazi zitalindwa. Mbali na hiyo Commission inayohusika na salaries na remuneration, kuna ile Commission ya Human Rights and Administration of Justice. Commission kama hiyo ndio uadilifu, sio uadilifu kumnyima mtu haki zake na mshahara wake. Kwa hivyo Commission itachungulia jambo kama hili. Mbali na njia nyingine kutakuwa na Ombudsman, kuna public protector, huyu pia anaweza kushtaki au kutumia njia ya kuhakikisha haki. Kwa hivyo tuna njia tatu, nne, kulinda haki za mfanyi kazi tofauti and that is to make sure that if one says there is another one.

Computerized elections: Tunaomba hivyo kwamba election zetu zitakuwa zile za computer. Juzi katika kutizama television nimeona jamaa mmoja anakwenda huko anatia kadi yake, anatia code kama vile code ya bank na automatically yake ile kura ishaingizwa kwa yule jamaa anamtaka yeye. Kwa hivyo hakuna haja ya kuhesabu kutoka kwa karatasi - hii ni kura ya fulani, hii ni kura ya fulani - it’s all automatic, yote iko mtambo ya computer na bila shaka Kenya itafikia hapo siku moja na haita kuwa mbali. Tukumbuke ya kwamba hii si Katiba ya leo au ya kesho au ya kesho kutwa, tutumaini kwamba itabakia miaka hamsini, miaka mia moja, miaka mia mbili na kadhalika, lakini tuombe kwamba itaharakishwa zaidi. Maana ya kwanza itakuwa ni njia nzuri ya saa hii ya kutegemewa kuhesabu kura kwa njia hii ya machine, hakuna mikono ya mtu ambaye inaingilia pale kuharibu. Pia itakuwa ni haraka zaidi na matokeo yanatokea haraka zaidi. Ikiwa mtu anapiga kura kati kati ya siku utaona kuwa katika eneo hili tutajua nani aliyeshinda maana yote inaingia kwenye machine na inajumlisha jumla inatokea pale.

Prime Minister ni swala nzuri, tuko on both houses. Prime Minister tuko katika National Assembly, ile National Council kazi yake itakuwa na speaker wake, itakuwa na members wake watajadiliana kama vile Uingereza. Uingereza Prime Minister Blair yuko House of Commons, wanajadiliana pale kila kitu na sheria ikishapitishwa pale inapelekwa House of Lords. Kule kuna wafanyi kazi wengine ambao ni leaders of Government Business. Yule Leader of Government Business katika nyumba ya pili ndiye atakaye-supervise majadiliano katika National Council.

Qualifications ya District Council hatukutaja hapo kwa hakika. Unajua kuna wale ambao wanasema kwamba utampata mtu ambaye labda ana degree lakini hana uwezo wa kuwatumikia wananchi. Kwa hivyo katika serikali ya wilaya wananchi wenyewe wanajua yule ambaye anaweza kuwatumika bora awe ni mtu ambaye ana ile commitment, ana nia ya kuwatumikia wananchi, ana nia ya kuwatumikia wenzake, ana uaminifu na kadhalika. Kwa hivyo hakuna haja ya mtu kuwa na degree au tuseme ‘O’ level ya aina hii au ile. Lakini huenda jambo hili likajadiliwa pia kwenye conference itakayofanyika kujadiliana juu ya Katiba na huenda ikabadilishwa na kuwe na qualifications pale. Hili ni pendekezo kwa hivi sasa hakuna haja kusema kwamba yule mjumbe katika serikali ya wilaya awe na elimu fulani, kiwango fulani na kadhalika.

Ndungu zanguni ninafikiri itabidi sasa kumaliza kikao chetu tumezidi kwa nusu saa. Bila shaka wako wengi kati yenu ambao mgependa kuuliza maswali, lakini ningependelea baada kunisikiza mimi kuwasikiza na wenzenu waliouliza maswala na kadhalika, mtarudia nakala zenu za Mswada wa Katiba na mtasoma vizuri. Lakini sisi tuko tayari ya kupokea maoni yenu ya kuandikwa mkitaka mtuandikie mimi nasoma section fulani, kifungu fulani katika Constitution, naona jambo hili lingefanywa hivi

na vile. Jeffa hapa na wenzake hapa wanakamati ambao mnawajua wanatoka katika eneo hili wanaweza kukusanya maoni yenu na kutupelekea Nairobi saa zile tunatayarisha huu mkutano mkubwa. Kwa hivyo mapendekezo yenu nyinyi raia wa binafsi yatachukuliwa pamoja na mapendekezo ya hiyo conference kubwa ili kuibadilisha hii Katiba. Sote pamoja tutaweka pamoja na kuzifikiria na kuzibadilisha hii Katiba kufuatia mapendekezo yenu. Hii ilikuwa ni kazi ambao nyinyi wenyewe mumetupa for the people driven constitution, nyinyi ndio mlitupeleka mbele kuifanya hii kazi – it is a people anchored Constitution. Msingi au nanga ya Katiba hii ni nyinyi raia, tumejaribu kadri tuwezavyo kuandika hapa mapendekezo yetu kufuatia mapendekezo yenu na tuombe huko mwisho hawa wajumbe wenyu watakao kuweko katika conference kubwa ya mia sita na hamsini ni wanjumbe wenu kwa hakika, sisi wanatume tutakuweko pale, wabunge wote kama nilivyosema waakilishi watatu. Kwa hivyo hakikisheni kwamba wale watakaowaakilisha Malindi District watatu, muwaeleze pia maoni yenu ili wakija kule wawasemee nyinyi wasijisemee nafasi zao and that will be the same with the other others. Na tuombe kwamba tutamaliza hii kazi kwa manufaa ya kila raia hapa nchini, mdogo, mkubwa, mlemavu, mzima, mama, baba, nyanya, babu, na tuombe kwamba tutaanzisha chapter au sura mpya katika tarehe ya nchi yetu, Mungu atusaidie asante sana.

**Jeffa Kingi (Coordinator):** Nipatieni muda kidogo niwafahamishe wale ambao watawakilisha wilaya ya Malindi katika ile kungamano ya kitaifa litakalofanyika Nairobi. Watu hawa walichaguliwa kwa kura ya siri ambayo ilifanyika Malindi. Waliochagua walikuwa ni ma-councillors wa county council ya Malindi. Tulikuwa tunatakikana tupeleke watu watatu kutoka kwa wilaya yetu na kati ya hawa watu watatu mmoja wao alikuwa ni awe ni mwanamke. Kwa hivyo mwanamke ambaye tutamtuma kutoka wilaya hii tulipata ni Zuhura Zukira Wanje ambaye amefika yuko hapa. Huyu alichaguliwa na atatuwakilisha kule Nairobi. Wengine ni wanaume wawili, wa kwanza ni Bw. Jilo Olutu. Wa pili anaitwa Sheikh Badawi ambaye ni mkazi wa Malindi. Hao ndio watatu ambao watakaotuwakilisha katika kungamano la kitaifa. Kama vile mlivyoambiwa kwamba tuna uwezo wa kujadili zaidi hii nakala ama mswada wa Katiba katika kila location tutakuwa na mkutano kama huu ambao wanakamati na mimi pia tutaenda hapa na pale kujaribu kujadili zaidi. Hakuna hata ungoje tuje huko chini, wewe mwenyewe vile umepata nakala unaweza ukasoma ukaandika memorandum kwamba sehemu fulani mimi ningependelea iwe hivi na hivi. Unaweza kumpatia mwenye kamati wa eneo lako ama unaweza kuja katika ofisi ya wilaya ukaweka pale ama mnaweza kukaa kama kikundi kama vile kundi la wanawake, mnaweza kukaa kama kanisa, mnaweza kukaa kama wanamsikiti mkajadiliana halafu mkaandika memorandum. Msingoje mpaka uje mkutano wa location, mnaweza kuanzia hivi leo, muanze kujadiliana na kuandika memorandum mwapatie wanakamati ama ikiwa una uwezo zaidi ukaleta katika ofisi ya wilaya. Sisi tutazisafirisha memorandum hizo mpaka Nairobi na maoni yetu hayataachwa nyuma. Tungependa kuomba kwa hivyo tungesihi mtu ambaye atajitolea kuja kutuombea dua, tuliombewa na Mkristo hapo mwanzo, tungeshukuru zaidi tukipata Mwislamu aje atufungie mkutano.

***(Prayer)***

Bismillahi Rahmani Rahim---------------------(in Arabic)

**The meeting ended at 1.45 p.m.**

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**